ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.

24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.

35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.

50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.

70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 29 Oktoba, 2009

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha hotuba kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007. naomba kuwasilisha.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007.

Mhe. Zahra Ali Hamad (Kny. Mhe. Abubakar Khamis Bakary - Waziri Kivuli wa Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007. naomba kuwasilisha.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu ombi la kuunda Kamati Teule ya Baraza chini ya kifungu cha 115 cha Kanuni za Baraza, kuchunguza malalamiko ya wananchi juu ya kunyimwa Vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 19

Chuo cha Mafunzo kuzungushiwa Ukuta Madhubuti

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo wakati mwengine hufanya shughuli zao mbali mbali ndani ya jengo la chuo.

(a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kuwa upande wa Kusini na Magharibi ya jengo hilo hakuna ukuta (*fence*) uliyo madhubuti wa kuwazuia wanafunzi hao wasikimbie?

(b) Je, wizara yako ina mkakati gani wa kukabiliana na suala hili, ili kuwanusuru Askari wetu wa Chuo cha Mafunzo na lawama zisizo za msingi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake Nam. 19 lenye vifungu a na b kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali inafahamu kuwa upande wa Kusini na Magharibi ya Jengo la Chuo cha Mafunzo Kilimani hakuna ukuta madhubuti. Kwa kuelewa hivyo, serikali kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo cha Mafunzo umeanza kujenga ukuta wa tofali ingawa kazi hiyo inaendelea kwa kasi ndogo kutokana na uchache wa fedha.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na jibu lake Mhe. Waziri zuri ambalo kanijibu na tunaamini kwamba litaleta muwafaka hapo baadae naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mwanafunzi chuoni au tuseme mfungwa ni binadamu, lakini na askari wanaepewa jukumu lile huwa ana kazi nzuri ya kumlinda binadamu mwenzake kutokana na mazingira magumu kama hayo niliyoyaeleza katika swali langu. Kwa kuwa jibu lake Mhe. Waziri kasema juhudi inaendelea kidogo si kwa kasi kubwa.

Je, Mhe. Waziri kwa kuzingatia hayo na usalama tuliokuwanao kwa vijana wetu wanaopewa jukumu la kuwalinda hawa wafunzwa, haoni kwamba kupunguza kasi kwa ujenzi huo kutawahatarishia usalama wao pindi akitoroka mfungwa na kupata adhabu ambazo hazistahiki?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, nakubaliana na wazo alilolitoa, lakini bado serikali inahudumia au inaweka ulinzi mzuri pale ukuta huo ambao ni mbovu kuhakikisha usalama wa wanafunzi waliokuwemo ndani ya Chuo cha Mafunzo hawakimbii. Kwa hivyo, tushirikiane na Mhe. katika kusimamia ujenzi huo ambao kwa sasa hivi unakwenda kidogo kidogo, lakini kwa kuwa ushirikishi wake utaweza kusaidia kupatikana fedha zaidi katika kutatua tatizo hili.

Nam. 70

Unyanyasaji wa Wafanyakazi katika Mahoteli ya Kitalii

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Tunaipongeza serikali kwa kukaribisha wawekezaji na kuitangaza nchi yetu kiasi ambacho wawekezaji wengi wakiwemo wajenzi wa mahoteli na wafanyabiashara mbali mbali wamewekeza na kuendeleza biashara zao nchini.

(a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kwamba wafanyakazi wa mahoteli wakiwemo wananchi wetu wananyimwa haki zao ikiwa ni pamoja na kufukuzwa bila ya utaratibu na kulazimishwa kufanya ngono na mabosi wao.

(b) Kama unalifahamu je, wizara yako imechukua hatua zipi ili kuwanusuru wananchi wetu na vitendo hivyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 70 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika naomba nitangulize maelezo machache kabla ya kujibu swali hili.

Mhe. Spika, napenda kukubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba juhudi kubwa zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeweza kuwavutia wawekezaji mbali mbali wa nje wa mataifa tofauti duniani kuja na kuwekeza Zanzibar katika miradi mbali mbali, aidha kuendeleza biashara zao.

Miradi hiyo imeweza kuisaidia Zanzibar na wananchi wake katika kuongeza pato la taifa kutokana na kodi; kuwapatia ajira wazalendo, pamoja na kusaidia huduma muhimu za kijamii na kadhalika.

Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kipengele (**a)** na (**b)** vya swali kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kumekuwepo na manung'uniko na malalamiko ambayo baadhi yake yamewasilishwa wizarani kwangu kutoka kwa baadhi ya wafanyakazi wa mahoteli, kwamba wanafukuzwa kazi na waajiri wao bila ya taratibu za kisheria

kufuatwa. Aidha, yapo madai kwamba baadhi yao hulazimishwa ki-ngono na mabosi wao.

Katika kipindi cha Januari hadi Oktoba mwaka huu, wizara yangu imepokea jumla ya madai au malalamiko 39 ya kufukuzwa kazi kwa Unguja na Pemba, ambapo hakuna madai ya maandishi yaliyowasilishwa yanayohusu kulazimishwa ngono na mabosi wao.

Malalamiko hayo yote yameshughulikiwa na wizara yangu na wadai 29 wamelipwa haki zao ikiwemo dai moja ambapo mfanyakazi amerejeshwa kazini. Madai 10 yanaendelea kushughulikiwa. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

	M/Magharibi	Kaskazini.(U)	Kusini (U)	Kaskazini. (P)	Kusini. (P)	
Madai yaliyopokelewa	21	8	8	2	0	39
Waliolipwa haki zao	14	8	7	0	0	29
Madai yanayoendelea kushughulikiwa	7	0	1	2	0	10

Wizara yangu imegundua kuwa wapo wadai/walalamikaji ambao makosa yao yanastahili kabisa kufukuzwa kazi kama makosa ya wizi, lakini waajiri mara nyingi huwa hawafuati taratibu za kisheria.

(b) Katika kukabiliana na matatizo haya, wizara yangu inachukua hatua zifuatazo:-

- Wizara imeongeza ukaguzi kazi sehemu za kazi ili iweze kufahamu kasoro mbali mbali zilizomo sehemu za kazi.

- Wizara imeendelea na kutoa elimu kwa wananchi kufahamu haki na wajibu wao kazini.

- Wizara inashirikiana na taasisi mbali mbali husika ikiwemo *ZIPA*, Uhamiaji, Kamisheni ya Utalii, Serikali za Wilaya na kadhalika kukabiliana na mambo yote ya uvunjaji wa sheria.

- Wizara yangu imeendelea na usimamizi wa sheria wa kusuluhisha migogoro hiyo kwa kuwarejesha kazini wale wote ambao wamefukuzwa kinyume cha sheria au kupatiwa maslahi yao ya kazi na inaposhindwa yote hayo, suala hili huwasilishwa Mahkama ya Kazi kwa hatua zaidi. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kufuatilia ukweli ulivyo juu ya matatizo yanayojitokeza katika sekta binafsi hasa mahoteli. Vijana wetu hao baada ya malalamiko kuyafikisha wizarani watendaji wake wanafuatilia na kupata haki kwa wale wanaostahiki, na kwa wale wanaobakia wanaendelea mpaka utaratibu utapopatikana ili wapate haki zao.

Lakini Mhe. Spika, katika vitendo vya rushwa ya ngono haya ni mambo ya ndani kabisa na siri. Kwa hivyo, nafikiri kweli maandishi patakuwa pahala ambapo hapana maandishi, lakini hivyo wakitokea wafanyakazi kama wanne au watano wanamlalamikia mtu mmoja tu kwamba anataka vitendo vya rushwa ya ngono ili tupate ajira. Mhe. Waziri haoni ni sababu tosha ya kumfanyia kazi mtu huyo anayehusika.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, wakitokezea watu na kulalamika kwa dhati kabisa kwamba wao wameombwa ngono ndio wapewe kazi, basi wizara haitosita kushughulikia. Lakini siku zote madai kama haya yanasemwa nje tu kurushwa rushwa, huwezi ukamtia hatiani mtu tu bila ya kuwa na taarifa ya kutosha na ushahidi wa kutosha. Kwa hivyo, wajitokeze wale wanaodaiwa ngono waseme sisi, na siku hizi tuna simu hizi basi acha simu zao wazitege hao wanaoambiwa kwa wanaowadai ngono.

Nam. 71

Elimu ya Dini Kuimarishwa kwa Watoto wa Zanzibar

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Kwa kuwa tuna vyuo vya Qur-ani na Madrasa mbali mbali zinazotoa elimu kwa watoto wetu nchini, na kwa kuwa elimu hii ni msingi mzuri na chachu ya maendeleo ya elimu ya sekondari na kukuza maadili mema kwa watoto wetu na wananchi wetu kwa ujumla.

(a) Je, wizara ina mikakati gani ya kuhakikisha watoto wetu wanashiriki na kupata kikamilifu elimu ya Qur- ani kwa maslahi ya maadili ya wananchi wetu kwa ujumla.

(b) Je, kuna vyuo vingapi vya Qur-ani katika Wilaya ya Mjini Unguja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, masuala ya elimu yanashughulikiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na hivi Vyuo vya Qur-ani pia vinasajiliwa na wizara hiyo hiyo kwa taarifa nilizonazo. Kwa hivyo, mipango ya maendeleo inayohusu vyuo hivi vya kuendeleza watoto itakuwa pia iko chini ya mamlaka hiyo hiyo. Ahsante.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni kweli kwamba masuala ya elimu yanashughulikiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini katika suala hili walimu wanaofanya kazi wanafanya kazi bila ya kulipwa.

Je, wizara yake kama wizara inayoshughulikia ajira, ana mpango gani wa kuona kwamba walimu hawa ambao wanafanya kazi kubwa na muhimu wanaingia katika utaratibu wa serikali kwa ajira.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nikiwa waziri mwenye mamlaka ya kusimamia mambo ya kazi, naamini kwamba sifurahii kuona watu wanafanya kazi na hawalipwi. Lakini kupanga namna gani walipwe hiyo ni mamlaka ya Wizara ya Elimu na nafikiri

watahakikisha kwamba hawa watu hawafanyi kazi bure na watalipwa mishahara.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2007

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likubali mapendekezo ya kuifanyia marekebisho Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar Toleo la mwaka 2007 kama ilivyopendekezwa na rasimu ya marekebisho ambayo imeshagawiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote.

Mhe. Spika, kwa furaha na heshima kubwa naomba kuchukua nafasi hii kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema. Pili nakushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, utaratibu wa kufanya marekebisho katika Kanuni za Baraza ni utaratibu wa kawaida ambao tunauendeleza mara kwa mara kukidhi matakwa na mabadiliko ya uendeshaji wa shughuli za Baraza, kutokana na uzoefu tunaoupata na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa kanuni hizo. Kwa mfano, mnamo mwaka 2005 tulifanya marekebisho ya kanuni, halikadhalika mwaka 2007 tulifanya marekebisho mengine ya kanuni na mwaka huu 2009 mwanzoni kabisa tulifanya marekebisho madogo ya kanuni, kwa kufuatia ile iliyokuwa ya Kamati ya Ufuatiliaji wa Ahadi za Serikali kuhamisha kazi zake za kamati hiyo na kuzipeleka kwenye kamati zetu za kisekta zinazosimamia utekelezaji wa wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena tunaomba kuleta mbele ya Baraza lako tukufu mapendekezo ya marekebisho ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi ili yaweze kujadiliwa na hatimaye yapitishwe ili yaweze kutumika katika taratibu za uendeshaji wa shughuli zetu za Baraza na kamati zake.

Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha Barazani mapendekezo haya ya marekebisho, tayari yalishawasilishwa mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kupata baraka za kamati hiyo kikamilifu.

Mhe. Spika, napenda kuishukuru sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu chini ya mwenyekiti wake Mhe. Haji Omar Kheir kwa kazi nzuri iliyofanywa na kamati ya kuchambua mapendekezo haya kwa makini

sana na kutoa maelekezo katika maeneo mbali mbali. Aidha, kumeshafanyika semina moja iliyowashirikisha wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kiasi kikubwa na walipata fursa ya kutosha ya kutoa michango na maoni yao ya kina kuhusu marekebisho ya kanuni hizo.

Mhe. Spika, naomba kuleta mbele ya Baraza lako hili tukufu mapendekezo yanayolenga kuzifanyia marekebisho Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar Toleo la mwaka 2007 kama inavyojionesha katika rasimu ya marekebisho ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari wameshapatiwa.

Mapendekezo ya Marekebisho haya ya Kanuni za Baraza yanatokana na kamati ya wataalamu ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi waliokaa na kufanya mapitio ya uchambuzi wa kina wa kanuni zetu zilizopo toleo la mwaka 2007. Na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya kanuni hizo ili ziendane na wakati na kuliwezesha Baraza letu tukufu kutekeleza ipasavyo majukumu yake kikatiba, kisheria na tuweze kulingana na Mabunge mengine ya nchi za Jumuiya ya Madola.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza sana wataalamu wetu, wanasheria wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa waliyoifanya kuweza kuichambua kanuni yetu na kuweza kufanya marekebisho mengi na hata pale kasoro ndogo ndogo za maandishi ambazo zilijitokeza wameona na wametuletea.

Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007, zinapendekeza kurekebishwa pamoja na mambo mengine ili ziweze kuweka utaratibu bora zaidi kwa uendeshaji wa vikao vya Baraza na kamati zake kwa manufaa ya wananchi na maslahi bora ya nchi yetu inayozingatia demokrasia na utawala bora. Aidha, baadhi ya marekebisho yanayopendekezwa kufanywa katika kanuni ili kuahikiana vizuri na zaidi ya masharti ya katiba pamoja na sheria nyengine za nchi. Halikadhalika haja ya kupanga vizuri mtiririko wa lugha pamoja na azma ya kukuza demokrasia ndani ya Baraza ni sababu nyengine muhimu zilizopelekea mapendekezo ya marekebisho ya kanuni hii.

Mhe. Spika, katika mapendekezo haya yaliyo mbele yetu, kuna jumla ya kanuni 72 zilizopendekezwa kurekebishwa. Kwa muhtasari nakala ya rasimu inapendekeza mabadiliko mengi ambayo baadhi yake ni haya yafuatayo:-

Katika kanuni ya pili inayohusu tafsiri na ufafanuzi yamefanywa marekebisho kwa kuongezwa baadhi ya maneno na kuwekewa tafsiri stahili. Aidha, baadhi ya maneno ambayo yalikuwa tayari yameshatafsiriwa, yamerekebishwa na kufafanuliwa zaidi ili kupata ufasaha wa lugha na kuchunguza maana kamili iliyokusudiwa.

Waraka wa marekebisho unapendekeza katika kanuni ya 10 kuwa Wenyeviti wa Baraza wawe wawili baada ya mmoja kama iliyo uchaguzi, na uchaguzi wao uzingatie jinsia. Pendekezo hili linalenga kutoa fursa ya jinsia kutoka uongozi wa Baraza. Hata hivyo, endapo itajitokeza waliojaza fomu kuomba kuchaguliwa kwa nafasi ya wenyeviti ni wajumbe wa jinsia moja tu, basi uchaguzi utafanyika kwa wajumbe hao waliyoomba hiyo nafasi.

Aidha, kuna mapendekezo yanayoletwa kwa ajili ya kuoanisha maneno yaliyotumiwa kwenye kanuni na yale yaliyotumika kwenye katiba. Mfano wa marekebisho hayo ni kanuni ya 59(10).

Mhe. Spika, katika mapendekezo hayo ya marekebisho ya kanuni, kuna marekebisho yanayopendekezwa ili kuondoa kasoro zinazoonekana kuathiri utekelezaji wa kanuni zenyewe. Mapendekezo ya aina hii ni pamoja na marekebisho ya kanuni ya 24 ambayo yanalenga kumpa uwezo Spika kuahirisha Kikao cha Baraza bila ya kuwahoji Wajumbe endapo shughuli za kikao zimekamilika mapema kabla ya kufikia muda wa kawaida wa kuahirisha Baraza.

Kanuni zinapendekeza kupitia marekebisho ya kanuni ya 62 kukataza wageni kuingia na simu katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi wakati wa vikao vya Baraza au kamati zake kama ilivyo hivyo kwa wajumbe. Hapo awali kanuni zilikuwa zinawakataza wajumbe kuingia na simu katika vikao vya Baraza na kamati zake, na kimsingi iliweka adhabu kwa mjumbe pamoja na mambo mengine kukatwa stahili zake za siku ya atakapoingia na simu yake, itaita au kuingilia mawasiliano katika Baraza. Bahati mbaya hakukuwa na utaratibu unaofanana na huu kwa wageni ambao simu zao zitaita au kuingilia mawasiliano katika Baraza.

Mhe. Spika, mapendekezo ya kanuni ya 73 yana adhma ya kuimarisha umuhimu wa uwekaji wa kumbukumbu ya mahudhurio ya Wajumbe kwenye Baraza na kwenye kamati. Aidha, mawaziri wanapokuwa wajumbe wa kamati hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kanuni ya 104 na 106 inapendekezwa kurekebishwa na kuongeza wajumbe wanne wa Kamati ya Uongozi wa shughuli za Baraza. Wajumbe wanaoongezwa ni mnadhimu kwa upande wa Chama Tawala, Mnadhimu wa Upande wa Kambi ya Upinzani na Wenyeviti wawili wa Baraza ambao watachaguliwa. Marekebisho haya pia yatapendekeza kuondoa ulazima wa kuwepo kiongozi wa shughuli za serikali kwenye Kamati ya Uongozi ili kukamilisha akidi ya mkutano huo. Kanuni ya 106 inajieleza.

Mhe. Spika, mapendekezo haya ya marekebisho pia yamefafanua majukumu ya kazi za kamati za kudumu za Baraza, katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma hususan kwa upande wa mapato na matumizi ya serikali katika wizara husika. Kanuni ya 107 hadi 110 inaeleza.

Mswada wa fedha ambao unakwenda sambamba na Bajeti ya Serikali nao unapendekezwa upelekwe kwenye kamati ya wenyeviti badala ya Kamati ya Fedha na Uchumi kama ilivyo hivi sasa. Kanuni ya 111 inaeleza.

Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* inapendekezwa ipewe uwezo zaidi inapopitia hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili ijiridhishe pia kwa kiwango cha fedha kinachotumika kulinganisha na thamani halisi ya kitu iliyofanywa au kitu kilichonunuliwa. Kanuni ya 112 inaeleza.

Mhe. Spika, marekebisho ya mapendekezo kuwa Spika atalazimika kukubaliana na ushauri wa Kamati ya Maadili na endapo atakuwa na mawazo tofauti atapaswa apeleke ushauri huo kwa Baraza kwa uamuzi wa mwisho. Kanuni 114 inaeleza.

Vile vile idadi ya wajumbe wa kamati teule inapendekezwa iongezwe kupitia marekebisho ya kanuni ya 115. Halikadhalika, inapendekezwa kwamba Mwenyekiti wa Kamati Teule awe na kura ya uamuzi tu bila ya kuwa na kura ya kawaida.

Mhe. Spika, kanuni zetu za sasa hazitaji wazi wazi ni pahala gani Spika na Makatibu Mezani watakaa ndani ya Baraza. Ili kuondoa dosari hii mapendekezo haya ya marekebisho yataeleza kikamilifu pahala ambapo Spika pamoja na Makatibu Mezani watakaa ndani ya Ukumbi wa Baraza.

Inapendekezwa kuwa utaratibu wa uchaguzi katika kuwatafuta Wajumbe wa Baraza wanaochaguliwa na Baraza ili kuwa Wajumbe wa Tume ya Bajeti urekebishwe ili wanaochaguliwa wasiwe Mawaziri, wala Manaibu Waziri, wala Wakuu wa Mikoa. Angalau mmoja wao pia awe ni mwanamke. Kanuni ya 143.

Mapendekezo haya yanalenga kuipa uhuru zaidi Tume hii kuzingatia usawa wa kijinsia katika vyombo vya kufanya maamuzi katika Baraza.

Mhe. Spika, mapendekezo ya marekebisho haya pia yanakusudia kupendekeza kuwa shughuli za Baraza katika kikao cha kwanza cha kila mkutano wa Baraza kitaanza kwa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar kabla ya kusomwa dua na kikao cha mwisho wa mkutano wakati wa kufungwa kwa Baraza kwa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar. Hii ipo katika marekebisho ya Kanuni ya 27.

Pendekezo hili linalenga kujenga utaifa na kukuza uzalendo wa wajumbe na wananchi wote kwa ujumla. Vile vile pendekezo hili linatoa ishara muhimu kwa shughuli zinazofanywa na Baraza Kitaifa.

Mhe. Spika, ukiachilia marekebisho haya ya msingi, mapendekezo mengine ya marekebisho ni ya jumla ambayo yanahusu zaidi kuweka vizuri mpangilio wa lugha, madhumuni ya kuzifanyia kanuni hizi zifahamike vizuri zaidi. Aidha, baadhi ya kanuni zinazojirudia rudia ama zimefutwa au zimeandikwa upya ili kuepusha kanuni moja kugongana na kutofautiana na kanuni nyengine.

Marekebisho mengine yanalenga kurekebisha mpangilio wa nambari na marekebisho ya makosa ya uchapaji Kanuni ya 8 na Kanuni ya 18 inaelezea.

Mhe. Spika, inapendekezwa kwamba endapo mapendekezo haya ya marekebisho yatakubaliwa na kupitishwa na Baraza lako tukufu, basi yaanze kutumika kwenye Mkutano ujao wa 18 wa Baraza hili tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kama nilivyosema mwanzo napenda sana kuwashukuru wataalamu wetu wanasheria wetu wa Baraza letu la Wawakilishi kwa kazi nzuri na kubwa waliyoifanya kwa kutuletea marekebisho haya ambayo yanalenga kuboresha kazi zetu kuwa za ufanisi zaidi katika Baraza lako tukufu la wananchi.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Haji Omar Kheri (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, awali ya yote naomba kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu bwana wa viumbe vyote, kwa kunijaalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, pia kuweza kutukutanisha tena Wajumbe wa Baraza hili ili kutekeleza kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Pili, nakushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi – Zanzibar.

Mhe. Spika, shukrani nyingi pia zimwendee Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi pamoja na Watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza hili Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim kwa kuweza kuwasilisha Rasimu hii mbele ya Kamati yetu kwa lengo la kuijadili na kutoa mapendekezo yake kwa yale maeneo iliyoona kuna haja ya kufanya

hivyo na hatimae iwasilishwe mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa kupata baraka na michango ya Waheshimiwa Wajumbe kwa lengo la kuuimarisha zaidi shughuli zetu.

Mhe. Spika, aidha, napenda kuishukuru tena Afisi ya Baraza la Wawakilishi – Zanzibar kwa kutupatia mafunzo ya siku moja ya kuitolea ufafanuzi Rasimu hii pamoja na kupokea mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kujadiliwa Barazani, ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waijadili Rasimu husika kwa umakini zaidi na hatimae watoe mchango au maoni yao kwa lengo la kuiimarisha zaidi Kanuni hii na kuleta tija kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipotoa pongezi na shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushirikiano wao mzuri waliouonesha wakati wa kuipitia Rasimu hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja mmoja baada ya mmoja;

1. Mhe. Haji Omar Kheri	Mwenyekiti
2. Mhe. Haji Mkema Haji	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Zahra Ali Hamad	Mjumbe
4. Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Mjumbe
5 Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Mjumbe
6. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	Mjumbe
7. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
9. Mhe. Najma Khalfan Juma	Mjumbe
10.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Mjumbe
11. Ndg. Nasra Awadh Salmin	Katibu
12. Ndg. Abdalla Ali Shauri	Katibu

Mhe. Spika, marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi sio suala geni katika Baraza letu hili, ambapo marekebisho kama haya yalifanyika mnamo mwaka 2005, 2007 na hivi sasa katika mwaka huu wa 2009 tupo katika mchakato huo. Lengo kuu la kufanya marekebisho haya ni kutaka kuimarisha zaidi Kanuni hizi, ili tuwe na Kanuni za kisasa zitakazoleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Baraza ukilinganisha na Toleo la mwaka 2007.

Mhe. Spika, kiujumla Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala iliridhika na kuyakubali marekebisho haya, hata hivyo, pamoja na kukubali kwake ilipendekeza baadhi ya marekebisho kwa madhumuni ya kuimarisha zaidi.
Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako kwamba mapendekezo ya Kamati yetu kuhusiana na Rasimu hii tayari yameshaingizwa kwenye Rasimu husika.

Hata hivyo, naomba niyataje baadhi ya maeneo ambayo Kamati yetu ilipendekeza kuingizwa kwenye Rasimu hiyo.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 27 cha Rasimu, kinachozungumzia Kanuni ya 72(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la 2007 (katika hotuba hii itakayojulikana Kanuni), katika mstari wa tano hadi mwisho kutoka juu maneno "kwa muda mfupi zaidi atakavyoona inafaa" yamefutwa na badala yake yamewekwa maneno "kinachofuata". Mhe. Spika, Kamati yetu ilipendekeza hivyo baada ya kuhisi kwamba Kanuni hii ilimpa mamlaka makubwa Spika hivyo anaweza kuyatumia mamlaka hayo visivyo.

Mhe. Spika, vile vile katika kifungu cha 39 cha Rasimu kilichozungumzia Kanuni ya 104 fasili mpya ya 7, Kamati yetu ilipendekeza kisomeke "Makatibu wa Kamati za Kudumu za Baraza isipokuwa Kamati ya Uongozi watateuliwa na Katibu wa Baraza kutoka miongoni mwa watumishi wa Baraza". Hii ni kutokana na kuwa mapendekezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati hii hayakueleza Makatibu hawa watateuliwa kutoka wapi. Hivyo, fasili hii ya Kanuni ingempa mamlaka Katibu wa Baraza kumteua Katibu Kamati kutoka sehemu yoyote aipendayo, ingawa jambo hili halijawahi kutokea, lakini Kamati iliona ni vyema mwanya huo ukazibwa mapema kama wahenga walivyosema "Kinga ni bora kuliko tiba".

Mhe. Spika, katika kifungu cha 62(i) cha Rasimu, Kamati ilipendekeza kuingizwa maneno "Naibu Spika na Mwenyekiti watavaa" baina ya maneno "Spika" na "joho" yaliyo katika mstari wa kwanza wa fasili ya (2) ya Kanuni ya 140. Hapa tunakusudia badala ya joho kuvaliwa na Spika peke yake sasa hivi kutakuwa na majoho. Kutakuwa na joho la Spika, joho la Naibu Spika na majoho ya Wenyeviti kwa kadri tutakavyoamua kuyachagua. Kamati ilipendekeza hili kuleta sura nzuri katika Baraza.

Mhe. Spika, sambamba na mapendekezo hayo Kamati pia, ilitoa pongezi kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuingiza katika Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni baadhi ya vipengele ndani ya vifungu kwa lengo la kuimarisha utendaji wa shughuli za Baraza. Baadhi ya vifungu hivyo ni; kifungu cha 25 fasili ya (ii) aya ya (a) na fasili ya (iii) aya ya (b) ya Rasimu hii, kimetoa fursa kwa Mjumbe Mkosaji kupewa nafasi ya kujitetea kama atakuwa na utetezi, endapo atafanya kosa kwenye Kikao cha Baraza au Kamati ya Baraza zima. Jambo hili linaashiria kukua kwa demokrasia katika Baraza la Kutunga Sheria - Zanzibar. Hii ni kutokana na kuwa Baraza litafuata moja kati ya *Principle of Natural Justice* ambayo ni haki ya kujitetea (kusikilizwa) *right to be heard.* Suala hili litasaidia sana katika kutoa maamuzi kwani Mjumbe Mkosaji ataweza kueleza ni sababu zipi zilizompelekea hata akafanya jambo au kitendo hicho na endapo Baraza litaridhika na maelezo yake anaweza kuepukana na adhabu hiyo.

Mhe. Spika, halikadhalika, Kamati yetu ilitoa pongezi kwa kufanyiwa marekebisho Kanuni ya 143 ambayo ni kifungu cha 64 cha Rasimu hii, kwa kutoa fursa zaidi kwa Waheshimiwa Wajumbe watatu wasiokuwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, wala Wakuu wa Mikoa *"Back Benchers"* kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza. Kamati iliunga mkono mapendekezo ya mabadiliko hayo kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe waliokuwa hawana dhamana nilizozitaja hapo awali ndio hasa wanaojua matakwa ya Waheshimiwa wasiokuwa na wadhifa Serikalini *"Back Benchers".*

Mhe. Spika, Kamati vile vile ilitoa pongezi kwa Watendaji wa Afisi ya Baraza kwa kupendekeza kwamba miongoni mwa Wajumbe hawa watatu basi angalau mmoja awe mwanamke. Jambo hili litaleta faraja kubwa hasa ukizingatia kuwa nchi nyingi duniani zimo kwenye mkakati wa kuinua maisha ya mwanamke. Hivyo, si vibaya na sisi Zanzibar tukawa katika mstari wa mbele juu ya suala hili.

Mhe. Spika, pongezi nyengine tulizitoa kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kupendekeza kuwa na Kamati mbili za Baraza zima ambazo ni Kamati ya Matumizi na Kamati ya Kutunga Sheria kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 9, kifungu cha 37 cha Rasimu ya Mapendekezo. Hivi sasa uzoefu tunapokaa kwenye Kamati zote zinaitwa Kamati za Baraza Zima. Sasa hapa tuna Kamati ya Matumizi na Kamati ya Kutunga Sheria.

Kwa mfano, kikao hiki kizima cha Baraza tulikaa kwenye Kamati ya Kutunga Sheria na sio Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, tuliona ni vyema zaidi hili jambo likapata ufafanuzi wa kikanuni kama nilivyoueleza.

Kamati ilitoa pongezi hizo kwa kuzingatia kuwa uanzishwaji wa Kamati mbili hizo kutasaidia kujua uhalisia wa ile shughuli inayofanyika kwa wakati ule ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, pamoja na marekebisho hayo Kamati ilitoa mapendekezo kwa baadhi ya mambo. Mambo yenyewe ni kama yafuatayo:-

- Kamati iliishauri Serikali kuzidi kuzitii Kanuni za Baraza la Wawakilishi hususan kwenye Kanuni ya 78(2) ya Kanuni hiyo ambayo inazungumzia kuwepo kwa tangazo la kwanza la Mswada wa Serikali angalau siku 21 kabla ya mswada huo kusomwa Barazani. Kamati imegundua kuwa mara nyingi Kanuni hii huwa haitekelezwi ipasavyo. Hivyo, inaiomba Serikali endapo Kanuni hii haiwezi kutekeleza basi ni vyema masharti ya Kanuni ya 79 inayohusu mswada wa dharura yakafuatwa ipasavyo. Kamati ilihisi hivyo, ili

kuondosha usumbufu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili sambamba na kwa Watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi – Zanzibar, kwani Afisi ya Baraza la Wawakilishi itapanga ratiba ya shughuli zake kwa umakini zaidi. Aidha, Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wamepata muda mzuri wa kujiandaa kwa kufanya utafiti kuhusiana na Mswada husika, lakini pia, kupata michango kwa Wadau mbali mbali kwa lengo la kuuimarisha Mswada huo, hususan wananchi wao waliowachagua.

Kwa upande wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, Kamati inawaomba Waheshimiwa hawa wazidi kuzitii Kanuni hizi kwa maslahi mazuri ya uendeshaji wa shughuli za Baraza. Kwani, Kamati yetu iligundua kuwa kuna baadhi ya Kanuni mara kwa mara huvunjwa na Waheshimiwa Wajumbe. Baadhi ya Kanuni hizo ni; Kanuni ya 62 fasili ya (4) aya ya (a) inayozungumzia matumizi ya simu ndani ya Ukumbi wa Baraza. Ili kuwafanya Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Wananchi kwa ujumla kuwa makini na ile shughuli inayofanyika ndani ya Baraza. Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wale wote wanaohudhuria kwenye Ukumbi wa Baraza kufuata masharti ya Kanuni hii.

Maana hiki kifungu cha Kanuni cha kutokuingia na simu na kutumika sasa hivi kipo kwa Wajumbe wa Baraza. Lakini inachoonekana bado tunaendelea kutumia simu ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kilichoongezeka ni kwamba hata kwa wale wasikilizaji. Kwa sababu kifungu kilichopo kilikuwa kinawabana Wajumbe, lakini kilikuwa hakikueleza wazi wazi kuhusu wasikilizaji au wageni wanaoingia kwenye Baraza.

- Imezoeleka kuwa Waziri na Naibu Waziri hushiriki kwenye vikao vya Kamati wakati wa kupitia bajeti na miswada ya Wizara zao pekee. Ili Kanuni ya 104 fasili ya (1)(b) ya Kanuni za Baraza itekelezwe ipasavyo, Kamati yetu ilishauri kuwepo kwa ushiriki wa moja kwa moja kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara husika wakati Kamati zinapofanya shughuli zake na sio kama ilivyo hivi sasa ni baadhi tu ya Mawaziri na Manaibu Mawaziri wanaoshiriki katika shughuli za Kamati wakati zinapofuatilia utekelezaji wa Wizara.

Kwa msingi huo, ni kwamba Mawaziri watakuwa ni wajumbe ambao watapata haki zote za Baraza isipokuwa tunapofuatilia shughuli za Baraza watakuwa wao hawapigi kura juu ya jambo ambalo litaamuliwa na Kamati. Waziri asiposhiriki katika shughuli hizo licha ya stahiki, ina maana ajieleze kwa nini hakushiriki kwenye shughuli hizo.

Mhe. Spika, namalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na pia kuniruhusu wewe Mhe. Spika, kwa mara ya pili kutumia muda mrefu kiasi katika kuwasilisha Maoni ya Kamati yetu. Mwisho napenda kutamka kwa niaba ya Kamati yetu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu naunga mkono Rasimu hii ya Mapendekezo ya Kanuni za Baraza la Wawakilshi - Zanzibar kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Zahra Ali Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2007.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu. Pia nachukua fursa hii kumuombea kheri Kiongozi wa Upinzani Mhe. Abubakar Khamis Bakary ambaye yuko Msumbiji kuangalia uchaguzi mkuu wa nchi hiyo ambao umefanyika jana.

Mhe. Spika, baada ya semina iliyofanyika Jumamosi 24/10/2009 mchango utakuwa mdogo sana kwa vile mengi kati ya maoni tuliyoyatoa yalizingatiwa. Hata hivyo, bado kambi yetu inahisi yapo maeneo yanayohitaji kuzingatiwa zaidi.

Mhe. Spika, Marekebisho ya Kanuni ya 27 ya Kanuni za Baraza yanaweka utaratibu wa kupigwa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika kila kikao cha kwanza na cha mwisho kwa Mikutano yote ya Baraza. Hili ni jambo zuri sana lakini hofu yangu ni kuja kuitwa mbele ya Kamati ya Mzee Ali Hassan Mwinyi Viongozi wa Baraza wanaotoka upande wa Chama Tawala. Je, wenzetu mmejizatiti na hilo? Sisi kwa bahati nzuri chama chetu kinathamini kinga ya kikatiba kifungu cha 86 (3) hivyo hatuna hofu yoyote.

Mhe. Spika, katika semina ya mapendekezo ya marekebisho ya kanuni iliyofanyika wiki iliyopita wajumbe hawakuridhika na utendaji kazi kwa wapambe wa Baraza na kupendekeza majukumu yao yatofautishwe na shughuli nyengine zinazohusiana na kazi zao. Majibu yaliyotolewa ni ya msingi na hayapingiki. Hata hivyo, tunasisitiza hili lifanyiwe kazi siku zijazo.

Mhe. Spika, Kanuni ya 69 ya Baraza inarekebishwa ambayo inahusu makosa na adhabu kwa wakosaji wakati wa vikao vya Baraza. Swali tunalojiuliza je,

kanuni hii haitapindwa pale ikiwa kwa bahati mbaya mjumbe aliyekosea anatoka upande wa Upinzani?

Mhe. Spika, katika semina ya marekebisho ya kanuni wiki iliyopita, baadhi ya wajumbe walishauri kanuni ya 143 ifanyiwe marekebisho ili nafasi moja kati ya tatu ya Wajumbe wa Tume ya Bajeti itoke Upande wa Upinzani. Kambi ya Upinzani bado inasisitiza suala hili lizingatiwe kwani hali ilivyo sasa haiendani na matakwa ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mhe. Spika, narudia tena kukukushukuru wewe binafsi na wajumbe wenzangu wote kwa kunisikiliza naunga mkono hoja.

Mhe.Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii kuwa mjumbe wa kawaida wa mwanzo kwa kuchangia marekebisho ya kanuni toleo la mwaka 2007.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, nimshukuru pia Katibu wa Baraza na Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika marekebisho haya na leo kuwasilishwa Barazani.

Mhe. Spika, katika umri wangu wa miaka 9 wa Baraza nimeshuhudia kama marekebisho mawili au matatu ya kanuni na wakati mwengine tunakaa kipindi kifupi tunarekebisha tena. Lakini kurekebisha Katiba, Kanuni, Sheria hizi ni kazi za Baraza wala hazina kwamba zimekuwa nyingi au sio nyingi, maana bila ya kurekebisha mambo huwezi kutengeneza mambo na ndio moja ya kazi yetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nianze japokuwa hoja zangu sikuziweka kifungu kwa kifungu lakini nafikiri nitaeleweka. Kwanza nianze na urekebishaji wa kanuni kifungu cha 27 kuhusu Wimbo wa Taifa.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono kuwepo kwa Wimbo wa Taifa katika Baraza hili kwa sababu ni kielelezo cha nchi yetu, lakini pengine kitaweza kuongeza hamasa na utii kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Ila naomba Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi. Je, huu wimbo utapigwa kwamba kutakuwa na chombo cha kupiga wimbo huu au Waheshimiwa Wajumbe tutaimba tu wimbo huu, sasa hili nalo ni muhimu kujulikana.

Mhe. Spika, pengine patakuwa na *CD* hapa inawekwa wimbo unapigwa halafu tunasimama sisi tunaendelea. Au kama tutaamua kwa kujizoesha kwa sababu tulipokuwa skuli tulikuwa tukiuimba basi moja kwa moja tutakuwa tunaimba wenyewe kwa kuongozwa na Spika, sina hakika itakuwaje.

Mhe. Spika, kifungu cha 24 kwa utaratibu ambao tulikuwa tumeuzoea Mhe. Waziri Kiongozi alikuwa akiomba Baraza kuahirishwa kama Shughuli za Baraza zimemalizika kabla ya wakati wake kwa kupitia Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, na Wajumbe wewe Mhe. Spika, ulikuwa ukiwauliza kama wameafiki au hawakuafiki, lakini mara nyingi wanaafiki haijawahi kutokezea kutokuafiki.

Sasa marekebisho haya nafikiri yanakwenda na wakati kwamba hivi sasa hakuna haja ya Mhe. Waziri au Wajumbe kuulizwa. Nafikiri Mhe. Spika, ambaye utakuwa na kiti hapo ukiona mambo yamekwisha unaahirisha Baraza tunakwenda zetu. Kwa hivyo, mimi hili naliunga mkono.

Mhe. Spika, kuna marekebisho ya kifungu cha 14 fasili ya kwanza (1) mimi nilitaka kujua tofauti yake nini, vile ambavyo kilikuwa kimeandikwa mwanzo na kilivyoandikwa sasa kuhusu Kiongozi wa Upinzani, maana yake kutakuwa na Kiongozi wa Upinzani ndani ya Baraza. Sasa ile fasili ya kwanza (1) ilivyoandikwa mwanzo na hii ambayo inataka kuandikwa sasa sina uhakika ni nini ambacho kimerekebishwa pale. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija kuzungumza hapa anifahamishe marekebisho haya yanalenga nini.

Mhe. Spika, niende kifungu cha 104 kwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, kwa Wajumbe wa Kamati wakati wa kazi za kamati katika wizara husika, lakini kutokuruhusiwa kupiga kura. Mhe. Spika, mimi naomba nilishawishi Baraza hili kwamba kwanza naungana na haya matakwa ya kanuni kuwa mawaziri washiriki kwenye kamati, kwa sababu ndio wanapata nafasi ya kuelewa kasoro pengine za wizara zao baada ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Maana yake unaweza kuwa waziri lakini usijuwe kasoro za watendaji wako au wizara yako yote. Lakini kwa kusaidiwa na Waheshimiwa Wajumbe ambapo ndio moja ya kazi yao ya kusaidia serikali basi utalijua tatizo lako liko wapi.

Mhe. Spika, mimi naomba kama Mhe. Waziri anapata stahiki zote za kikao au za kamati, kwa nini asiruhusike kupiga kura na kama waziri hata awe na Naibu Waziri watakuwa watu wawili hawatoweza kubadilisha maamuzi ya kamati. Wenzetu katika Bunge mawaziri wanapiga kura kwenye kamati, zaidi wakati wa kuchagua uongozi wa kamati. Sasa kwa nini hapa tuwabane mawaziri wasipate fursa hii ya kupiga kura wakati na wao ni wajumbe wa kamati.

Mfano kamati ina wizara mbili mpaka nne, lakini kwa yale mambo ya jumla basi wapige kura, kama yale ya wizara yake kuchunguza vitu yale yasipigiwe kura, lakini hapa hata tukiletewa kamati nzima ya Baraza mawaziri wanapiga kura, kwenye shughuli zote za Baraza mawaziri wanapiga kura, hatujaambiwa nyinyi mawaziri msipige kura. Kwenye kamati kwa nini tunaambiwa tusipige kura.

Kwa hivyo, mimi nahisi na mawaziri nao madamu wana haki ya kupata fursa kwenye kamati, basi na wao wapate fursa ya kupiga kura. Vyenginevyo tuambiwe kwamba wakipiga kura wataharibu mwelekeo gani katika kamati.

Mhe. Spika, katika kanuni ya 106 Kamati ya Uongozi. Mhe. Spika, mimi nashukuru kwamba Baraza limekubali kuwa na wenyeviti wawili na kwa jinsia, pengine hii itapunguza mambo yetu kuyumba yumba, kwa sababu tunakuwa kidogo. Lakini katika kanuni hii jambo ambalo naliona kwangu mimi sio jema kupanua wigo wa Kamati ya Uongozi ya Baraza, kuwaingiza Wanadhimu wa vyama kuwa wajumbe wa kamati ya uongozi, mimi siungi mkono. Kwa nini?

Mhe. Spika, kwenye kamati ya uongozi ya sasa kiongozi wa shughuli za serikali yumo, kiongozi wa upinzani yumo. Kwa hivyo, sioni kwa nini na wanadhimu wa vyama waingie humo. Ningependa kamati iendelee na mfumo ule kwamba wenyeviti wa kamati, kiongozi wa shughuli za serikali na kiongozi wa upinzani, Spika na Naibu Spika, basi tuendelee hivyo. Sasa tukienda huko, Baraza lenyewe hili ni la wajumbe 80 kamati ya uongozi ya wajumbe 20. Sasa inakuwa kama timu ya taifa ya zamani, wachezaji 6 wa riadha na viongozi 14 wanaelekea Rome. Kwa hivyo, gharama za uongozi ni kubwa timu haifanyi vizuri.

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi nahisi tusiitanuwe sana hii kamati ya uongozi, bado nahisi inafanya kazi nzuri. Hawa wanadhimu kwa heshima zao, kwa upande wetu najua kwamba, kwa vyovyote mnadhimu wetu hatuwezi asiwe mwenyekiti wa kamati hata siku moja, kwa sababu tunampa heshima hiyo. Kwa hivyo, na yule mnadhimu wa upande wa upinzani ajitahidi awe mwenyekiti wa kamati, lakini haiwezekani tena aah! Jamani huu mchuzi si utakuwa na pilipoli nyingi. Nawashawishi wajumbe wenzangu kwamba tungewaondoa hawa wanadhimu kwenye kamati ya uongozi. Timu yetu ni ndogo sana ya uongozi, na uongozi utakuwa mkubwa sana, hawa wanadhimu watafutiwe njia nyengine waingie lakini sio kwa sababu ya nafasi zao za vyeo.

Kwa hivyo, mimi naomba tungeendelea na utaratibu ule wa zamani. Labda tungewaongeza hawa wenyeviti wawili ambao wameingizwa, hawa naunga mkono, lakini tusiwaingize wanadhimu kuwa wajumbe wa kamati ya uongozi.

Mhe. Spika, kanuni 143 marekebisho ya kanuni. Mhe Spika, najua kwamba kati ya wajumbe watatu waliochaguliwa na Baraza hili wa kamati ya bajeti, kwa bahati nzuri sio mbaya, sasa ni mawaziri, isipokuwa mmoja. Pengine atakuja na yeye, ndio maana ikaja hoja hii.

Mimi ni mmoja ya wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Nilipochaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti nilikuwa *back bencher*. Sasa naunga mkono kwamba mawaziri waondolewe kwenye Kamati hii. Kwa sababu wakati mwengine, mimi mwenyewe nimejiona nakuwa nashindwa kwenda kuwatetea wawakilishi inanibidi niitetee serikali kwa sababu ni waziri. Maana kamati ile nayo ina kazi ngumu, ile ni kama kwenda kumchinja mtu, pale mjali maslahi ya waheshimiwa.

Kwa hivyo mimi naunga mkono kwamba mawaziri wasiwemo kwenye Kamati ya Bajeti wale watatu, walioingia kwa nafasi zao za uwaziri waendelee kuwemo ili wakaitetee serikali kwa sababu ni lazima na serikali itetewe nayo.

Lakini je, huu uchaguzi utafanyika tu baada ya Baraza kuundwa au tutasubiri kwanza Baraza litangazwe halafu ndio tuanze Baraza. Maana vyenginevyo itakuwa tutakuwa tunajiuzulu kila wakati.

Jambo jengine la kamati hii Mhe. Spika, waheshimiwa kwenye kamati za wenyeviti na makamo wenyeviti wana posho maalum la nyadhifa. Lakini hawa wajumbe watatu wa kamati ya bajeti ambao wanafanya kazi kubwa hawana posho la nyadhifa kwa nini, na wao watakuwa ma-*back benchers* kwa nini wasiwe na maposho ya nyadhifa. Kwa hivyo, mimi naunga mkono kuwa mawaziri waondolewe, lakini na hao ma-*back benchers* watakaoingia kwenye kamati ya bajeti wawe na posho ya nyadhifa na wao kama wenyeviti wa kamati. Maana hata hiyo bajeti ya wenyeviti wa kamati na Baraza zima wanaipitisha wao, hivi kwa nini wao ambao wanapitisha, wanauza samaki wasile samaki. Spika, ana posho la nyadhifa, kiongozi wa serikali ana posho la nyadhifa na hawa watatu kwa nini wanatulinda sote humu, basi hawa nao waingizwe kwenye posho la nyadhifa kuanzia bajeti ya mwakani.

Mhe. Spika, kuhusu jinsia naunga mkono kwamba moja kati ya watatu hawa awe ni jinsia nyengine, huwezi kusema mwanamke, kwa sababu inawezekana wakawa wanawake wawili na mwanamme akawa mmoja. Lakini siungi mkono hili la msemaji wa upinzani alisema kwamba tuangalie vyama. Suala hili mimi naona halina maana na wakati mwengine tuepuke sana mambo haya ya kuangalia vyama humu Barazani, bora tutazame jenda, ili tunusuru Baraza letu liwe na utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli zake. Nina hakika tukikubaliana vizuri basi pande zote watapata kura katika hili.

Mhe. Spika, jengine ni hili la waalikwa wa Baraza na kuhusu simu zao. Ni vyema kuwepo kipengele hiki, lakini tupewe matoleo kabisa ili tuwazoeshe watu wetu wasije wakapata adhabu za Baraza. Maana yake wanapokuja hapa Barazani wanapaogopa, wanasema humu Barazani kama jela, wakiingia humu wanajiona kama wako jela, sasa wakipata na shughuli nyengine humu zitawatisha zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, utatumia busara yako ili kuweka mambo sawa.

La mwisho Mhe. Spika, kwa sababu mimi ni mchangiaji wa mwanzo baada ya msemaji wa kambi ya upinzani, basi niseme kwamba kamati ya Mzee Mwinyi haikuwa na madhara kwetu. Yale ni maamuzi ya chama, hatukuenda kufanya jambo baya wala kubwa ambalo halipo. Kwa hivyo, tumekwenda kufanya shughuli za chama chetu, ambapo kama chama cha upinzani wanafanya shughuli zao, na humu Barazani wanafanya wakati mwengine wanasusia, wananuna kama siku moja au mbili halafu wanarudia tena, yaani hayo ni maamuzi ya chama tu. Kwa hivyo, yale yanapita na kurudi tena. Sisi nafikiri hatukufanya jambo baya. Tumefanya jambo zuri na ndio maana tuko humu vizuri, kwa maslahi ya chama chetu, kwa maslahi ya nchi yetu na nafikiri tutaendelea kushirikiana vizuri. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na mimi asubuhi hii ya leo Mwenyezi Mungu kutujaalia tukawa wazima na tukafikia hapa ambapo leo tupo, tukijadili mambo muhimu ambayo yanatuhusu pamoja na wananchi wetu.

Mhe. Spika, sitokuwa na mchango mkubwa sana, lakini nitataka kudondoa mambo mawili au matatu na pengine kutoa shukurani kwa hayo hayo mawili au matatu pia ambayo yamejitokeza katika marekebisho haya ya kanuni za Baraza kwa mwaka 2009.

Mhe. Spika, nina wingi wa furaha na shukurani za dhati kwa kukubalika wazo la kuionesha Zanzibar kwamba nayo ni nchi. Sifa za nchi Mhe. Spika, ni pamoja na kuwa na chombo cha kutunga sheria kama hiki chetu, ambacho kinaitwa Baraza la Wawakilishi. Pia kwamba tuna bendera, kuna Rais. Kwa hivyo, ni vyema kwamba kwa sababu na wimbo wa taifa wa nchi hii upo, kama alivyozungumza mwenzangu aliyekaa kitako yeye alipokuwa shule, lakini mimi likuwa skuli tulikuwa tukiuimba wimbo huu.

Unajua Mhe. Spika, watoto wanapokuwa wanaimba, wanakuwa wana hamasa. Kwa hivyo, na sisi tumefurahi sana kwamba leo tutawasaidia watoto wetu kukumbushia hadhi ya nchi hii kwamba ina wimbo wake wa taifa. Mimi nilikuwa nikiumia sana kuona kuwa tulikuwa tunaimbiwa tu siku zote, watu wanaimba wimbo wao lakini wanasema wetu sote. Inawezekana labda, lakini

mimi nasema Zanzibar kama nchi basi tuna wimbo wetu wa taifa, na hili natoa shukurani kabisa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu hii kamati yetu ya uongozi. Kama ilivyozungumzwa hapa wenzangu wanasema kwamba wao wanaona kamati ni kubwa wameongezwa watu wanne, lakini wao wanahisi kuna wawili wapunguzwe.

Mhe. Spika, mimi nilitoa mawazo yangu wakati wa semina, nadhani Mhe. Mjumbe aliyekaa kitako sasa hivi kama hakuwepo vile kutokana na maswali yake. Lakini muhusika atakuja kumjibu maswali yake ambayo ameyatoa hapa. Mimi nilishauri kwamba ni vyema kujaribu kukwepa gharama kadiri itakavyowezekana, kwa sababu kama tunavyojua hali halisi ni kwamba tuna upungufu wa fedha katika nchi, kama linavyozungumzwa suala la pesa kidogo ni matatizo. Sasa marekebisho yake mimi nadhani, sikatai hili suala la kuwa hii kamati ni kubwa. Kwangu mimi nina mawazo mengine, sio kupunguzwa hawa walioingizwa. Mimi nadhani hawa walioingizwa wako sahihi kabisa kuingizwa hawa watu wanne.

Lakini Mhe. Spika, ukubwa wa kamati ile umetokana na utaratibu wa namna ya kupata viongozi katika Baraza na nikapendekeza na sasa hivi nitarudia tena kupendekeza kwamba tunapochagua Spika, atakapotoka Spika, upande wetu sisi basi upande we wenzetu watowe Naibu Spika. Lakini utaratibu ambao tulikuwa tunauchukua, ulikuwa tunampigia kura mmoja mmoja, kwa maana hiyo wingi wa kura unatoka upande mmoja tu, kwa hivyo, Spika atatoka kwao, Naibu Spika atatoka kwao, Mwenyekiti atatoka kwao na kungekuwa na mpambe wa mwenyekiti na mpambe wa Spika basi wote wangetokea kule.

Kwa hivyo, mimi nadhani kwa ile ile nia njema tunayoizungumza katika vikao vyetu vya Baraza hili tukufu basi kuwe na utaratibu mzuri, kwamba akitoka Spika, upande mmoja Naibu wake atoke upande wa pili. Halikadhalika wale wenyeviti wawili. Hii itaondosha budhdha ya kuwa na kundi kubwa kama wanavyolalamika wengine. Huo ndio ulikuwa ushauri wangu katika suala hili. Kwa sababu kuongezeka huku tungejiuliza au Mhe. Mjumbe aliyekaa kitako pengine na wenzake wenye mawazo kama yeye, wangejiuliza kwa nini waliingizwa hawa. Sio suala la kwamba tumewaongeza tu, lakini ilikuja mantiki ya kuonekana na ikakubalika ndio maana ikafikia watu wale kuongezwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana ili hiyo kamati iwe ndogo kiasi itakavyokuwa na ile hoja ambayo ilijengwa mpaka ikabidi iongezwe hao walioongezwa basi ingeangaliwa vizuri, kwamba katika upatikanaji wa

viongozi wa Baraza, basi kuwe na utaratibu mzuri wa kuona pande zote mbili zinawakilishwa katika uongozi wa chombo hiki.

Mhe. Spika, nikitoka katika hiyo. Nije katika marekebisho yake ya kingu cha 143, nilikuwa naweka msisitizo tu, kama ambavyo kambi yetu tumeona kwamba wale wajumbe watatu watakao kuwa wa tume ya bajeti basi angalau mmoja awe mwanamke, nakubaliana nayo. Pia isionekane ni ya chama kimoja, wala suala hili halitaleta mvutano wala chochote. Tukiwa sote pamoja kila mmoja ana namna yake ya kuwakilisha kwenye tume ile, na tutakwenda vizuri tu. Nadhani hiyo haina hoja wala mjadala ni suala la kutumia nia njema tukazingatia kwamba sote tunahitaji kuwakilishwa katika kila sehemu. Kwa hivyo katika nafasi tatu zile moja ikawa inatoka upinzani, lakini ndani ya nafasi tatu zile basi japo mmoja awe mwanamke, hii naiunga mkono mia kwa mia Mhe. Spika.

Suala jengine Mhe. Spika, ambalo naomba nilizungumze ni kuhusu vazi la Mhe. Spika, na wenzake. Kama sikosei ni katika kifungu cha 140 halikufafanuliwa vizuri, mimi kidogo nilikuwa nataka nijuwe litakuwa ni la aina gani, tungejua zaidi litakuwa vipi kwa sababu nina hofia kidogo likijakuwa halikupendeza. Sio rangi Mhe. Spika. Mhe. Spika, sikusudii rangi yake, rangi inaweza ikawa rangi yoyote ambayo tutakubaliana. Bahati nzuri imetajwa kabisa itakuwa ni rangi ya *blue dark* na umependeza Mhe. Spika, pamoja na makatibu wetu. Mhe. Spika, nilikuwa ninauliza aina ya hilo vazi sio kwa maana ya rangi lakini ile *design*.

Mhe. Spika, unajua kuna *design* ambazo nyengine linaweza likawa zuri, lakini watu, sio wakalidharau lakini likawavunja moyo sijui kitu kama hicho, kwa sababu kuna mavazi ya mapadri nayo yako kama majohomajoho. Kwa hivyo, ninahofia Mhe. Spika, usije ukavaa la aina ile kwa sababu misingi yetu ya kidini ingawa hatuangalii udini, lakini ni lazima tujitazame pia mavazi. Kwa sababu wakati mwengine vazi linakuwa *identify* kabla hujasema kitu. Kwa sababu Waafrika tunasema tuko wamoja na kila kitu, sasa wakati mwengine ukija ukivaa vazi la mwenzio unaonekana na wewe uko upande ule kumbe sio. Kama ilivyokuwa wengine hawawezi kuvaa kofia na kanzu na koti kama anavyopenda kuvaa Mhe. Mjumbe pale.

Sasa nadhani kadiri itakavyowezekana vazi la Mhe. Spika, basi kwanza liwe lina sifa mbili kubwa. Sifa ya kwanza atakapoonekana basi aonekane kama ni Mzanzibari, yaani aweze kuwa tofauti na mwengine ambaye si Mzanzibari. Sifa ya pili iwe ni hiyo mtu asijeakaona kama huyu anatokea kwenye madhahebu yale ya wenzetu, lakini kumradhini nilikuwa naomba sana tuliangalie vazi la Mhe. Spika, wa Baraza la Wawakilishi la chombo cha kutunga sheria cha nchi ya Zanzibar, basi iwe linatoa hiyo haiba na

kumtambulisha kabla ya kusema. Kama ambavyo tunaona mikutano ya kimataifa Mhe. Spika, akija Msudan, basi unajua kuwa yule ni Msudan kwa kilemba chake na akitokezea jamaa zangu wa Comoro basi unajua wale ndio. Halikadhalika pia akija Muoman unamjua kama yule ni Muoman. Kwa hivyo na mimi nilikuwa naomba sana kuweka msisitizo kuwa vazi la Mhe. Spika, wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar basi liwe linatoa haiba hiyo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi naomba ufafanuzi katika hoja ndogo tu ambapo Mhe. Mjumbe aliyekaa chini sasa hivi ameizungumza.
Mhe. Spika, hoja yangu ni pale ambapo patatokea mabadiliko, mfano kama Spika hayupo au Naibu Spika hayupo au Mwenyekiti hayupo. Sasa mwenzetu ametushawishi kidogo tukubaliane kwamba upande huu ukitoa Spika, na upande ule wa kambi ya upinzani atoke Naibu Spika. Mimi nilitaka kujua kidogo. Kuna wakati wenzetu wanafuata chama hawafuati Baraza la Wawakilishi. Je, ikitokea siku hiyo wamepangiwa wao Mwenyekiti atuongoze sisi, hawajikutuacha sisi wana CCM peke yetu ndani ya hili Baraza, maana yake hii ndio hoja yangu kubwa. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Spika, mara nyingi huwa tunaona tunaweza tukaingia ndani ya ukumbi Mhe. Spika, tukajikuta tuko peke yetu upande huu wa CCM. Mfano, siku hiyo ndio tunataka kuongozwa na kiongozi anayetokea upande wa upinzani na wapinzani wamesema leo ni siku ya kuwa wakaenje tu wasiingie Barazani. Saaa kwa nia ile ile ambayo ameizungumza mjumbe ni kwa nia safi, basi mimi nawashawishi wenzangu wasikubaliane na nia hiyo, mpaka pale ambapo wenzetu watatuthibitishia kwamba sasa watakuwa ni wajumbe wa Baraza sio wajumbe wa chama chengine. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Spika, labda tumemsikia mjumbe mwenzetu akisema kwamba yeye alisoma skuli na Mhe. Machano alisoma shule. Naomba niweke sawa, ninavyofahamu mimi kwa sababu nilisoma Kijerumani kidogo, *"s c h u l e"* inatamkwa neno shule. Sasa Wajerumani wanaita shule na Waingereza sisi tunalainisha lugha tunaita skuli, kwa sababu wenzetu kule Tanzania Bara wengi walitawaliwa na Wajerumani. Kwa hivyo, ni tafsiri mbili, ukisema shule uko sahihi na ukisema skuli uko sahihi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Yaani, Mhe. Khatibu ana wasi wasi kwamba hata kiti kitakuwa wazi siku hiyo. *(Vicheko).*

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Ahsante Mhe. Spika, hoja yangu kidogo Mhe. Khatib aliichukua. Lakini nafikiri utaratibu unatueleza kuwa Spika, Naibu Spika, hata wenyeviti watachaguliwa kwa kura. Sasa tusivuruge

demokrasia ambayo imo katika Baraza letu kwa kusema tutowe mmoja huku na mmoja huku, twende kwa kura.

Mhe. Spika, wenzetu wawe hodari wa kupiga kampeni ili wakubalie na wapate kura, basi waingie. Lakini vyenginevyo itakuwa tunavunja demokrasia ndani ya Baraza letu na mengine Mhe. Khatib aliyazungumza vizuri.

Mhe. Spika, mimi niko katika kanuni ya 59(8)(b) naomba kunukuu:

Kanuni ya 59(9)(b)

> "Kutumia haki yake ya kusema kwa madhumuni ya kutaka kucheleweshe shughuli za Baraza".

Mhe. Spika, hoja hii mwaka jana Mhe. Ali Suleiman Ali aliitoa, lakini wakati ule alikuwepo Mhe. Mwanasheria Mkuu, akamwambia hapana, hapa tunazungumzia kwenye kamati sio kwenye Baraza. Tulipokuja kukaa na kutizama maana ya Baraza, inasema maana yake ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lililowekwa kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar na inajumuisha kamati ya Baraza zima na kamati nyengine yoyote. Kwa hivyo, ikiwa kamati ya Baraza ama kamati nyengine yoyote hii inatumika.

Mhe. Spika, hoja yetu ilikuwa kwamba wakati unauliza waliokubaliana na makadirio haya, tunanyanyua mkono, wanaokataa wananyanyua mkono. Sasa ilikuwa kwamba kama mtu amekataa kanyanyua mkono kwamba kakataa katika vifungu anasimama anapiga buti na kutaka apate maelezo, hiyo sio kupoteza muda. Lakini nilipoileta hoja hii na mimi wakati mwengine ukaniambia hapana na nafasi ya kutumia kifungu ukanitajia sijui kifungu cha ngapi vile.

Sasa hoja yangu Mhe. Spika, kifungu hiki na kile hakiingiliani, ama hii kucheleweshe Baraza inakuja kwa wakati gani. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, mimi nina swali dogo sana. Swali langu ni katika kanuni ya 91,92 na 93 ni kuhusu masuala ya utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha.

Mhe. Spika, nilipoangalia haya marekebisho ya kifungu cha 92 nilidhani labda Mhe. Waziri angetupa yale marekebisho ambayo katika mkutano uliopita wa bajeti tulizungumza, ni suala ambalo linahusiana na *finance bill* na *appropriation bill*. Tuna tatizo kidogo na wenzetu Bungeni wamerekebisha hili, kwamba sisi tunatunga *finance bill* mwisho wa kikao ambapo masuala ya kodi yameshazungumzwa na serikali kwamb yangebadilika kwa njia moja ama nyengine.

Mhe. Spika, mwaka wa fedha unaanza mwezi wa Julai na Baraza linamaliza mwezi wa Agusti. Sasa sisi tunaposema kwamba tunapitisha *finance bill* mwezi wa Agusti au Septemba ni kwamba hii miezi mitatu ya kuanzia mwezi Julai mwanzo ambapo ndio kodi zinatakiwa zibadilike pale tunayumba, kwa sababu hatujui tunafanya nini. Kwa sababu *finance bill* haijakubalika kuruhusu kodi zikusanywe kwa mujibu wa mabadiliko, itakuwa tunakwenda kinyume na sheria, sheria ya *finance* huwa bado haijabadilishwa. Kwa hivyo, mimi nilidhani marekebisho haya ya kifungu cha 92, utaratibu wa kutunga sheria za fedha ingewezesha kwamba tutunge *finance bill* mara mwaka wa fedha unapomalizika, yaani tarehe 30 Juni ikimalizika, basi tulete pale *finance bill*, halafu mwisho ndio tunatunga *appropriation bill*.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri kwamba haya ni marekebisho muhimu na kwa sababu tunarekebisha hii kanuni, basi ningemuomba Mhe. Waziri kama ana muda basi aiangalie ili tuyapitishe Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi kwa masuala mengine bado naungana na utaratibu ule wa kwamba wanadhimu waingie katika kamati ya uongozi. Suala hili Mhe. Spika, ni muhimu sana kwa sababu wanadhimu ni muhimu sana katika kambi zetu na wanasaidia sana katika masuala ya kuimarisha nidhamu na mambo mengine ya kuwasaidia viongozi wa kambi zetu katika ama kiongozi wa upinzani ama Waziri Kiongozi. Hili ni suala muhimu sana ambalo nahisi bado tuendelee kuwa nalo. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Hivi kuna mwenzetu anakoroma humu ndani, sawa *(Vicheko).*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliwa kuwa wazima na kuweza kuhudhuria katika kikao hiki cha Baraza.

Mhe. Spika, na mimi nina mchango mdogo tu. Mchango wangu kwanza ningeuelekeza katika maeneo karibu mawili ama matatu. Katika kupatikana kuchaguliwa kwa Spika, Naibu Spika na wenyeviti. Mhe. Spika, naona kwamba nimuhimu na ili demokrasia itumike basi utaratibu uliopo ufuatwe, kwa maana ya kwamba watakaoshinda kwenye kura zile za uchaguzi awe ndio amepita, bila kujali kwamba huyu anatoka chama gani na huyu anatoka chama gani. Kama atashinda kutoka upande wa wenzetu sawa na kama atashinda kutoka upande wetu iwe sawa. Lakini kusiwe na mapendekezo kwamba lazima atoke mahala fulani.

Mhe. Spika, jengine ambalo naomba kuchangia na mimi naunga mkono ile hoja ya kuwaingiza wanadhimu katika kuwa wajumbe naona haina ulazima. Mhe.

Spika, mimi napendekeza kwamba suala la kusema Mnadhim wa Chama cha Mapinduzi na Chama cha Upinzani wawepo pale kisheria, sioni mantiki. Kwa hivyo, hiyo napingana nayo.

Aidha, kama itakuwa wameingia kwa sababu ya njia nyengine kama vile Mwenyekiti wa Kamati sawa hakuna tatizo, lakini kama tunaiweka kwa mujibu wa Kanuni kwamba tunapendekeza hivyo. Kwa kweli sikubaliani na hoja hii.

Mhe. Spika, mengine yote ambayo yamependekezwa sina matatizo nayo. Isipokuwa maeneo hayo mawili nimeyaangalia na kutizama uzito wake sikuona.

Kwa kweli Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira ametusaida kwa kiasi fulani katika maeneo yetu haya ambayo tulikuwa tukiyazungumzia. Mhe. Spika, ni kweli kwamba wenzetu mara nyingi wanazungumzia nia njema, lakini katika nia njema hiyo haionekani humu ndani ya Baraza.

Kwa mfano, tunakuwa tunapitisha mambo mbali mbali na tunapofikia maamuzi wanaokubali wao wanakaa kimya, na pengine mtu ametoa mchango mzuri na Mhe. Waziri ameyakubali mapendekezo yake. Lakini kutokana na misimamo ya chama anarudi kwenye chama chake.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema ili kuona tusijekufika pahala tunaathiri Baraza letu tunakuja kwenye kikao hapa na tayari ameshapangwa pengine Mwenyekiti au Naibu Spika, ambaye anatoka upande wa wenzetu (Upinzani). Hivyo, wakati umefika akaamua kubaki njiani na kuachwa solemba katika baraza, nafikiri suala kama hilo si zuri na wala halitaleta ufanisi wa kazi zetu. Kwa hivyo, kwa kuepusha hilo nadhani ni vizuri utaratibu uliopo uendelee.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nikatoa mchango wangu kidogo kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Kwa upande wangu nitazungumzia maeneo mawili, ambayo maeneo yote nitakayoyazungumzia napendekeza kuongezwa baadhi ya mambo au maeneo haya katika Kanuni yetu mpya ambayo tunategemea kuipitisha hivi sasa.

Mhe. Spika, katika Kanuni yetu iliyopita kifungu cha 59 kinazungumzia mambo yanayofaa na yasiyofaa kuzungumzwa, ambapo kuna kifungu cha 59, yaani vifungu vidogo vya 59 kuanzia 1 mpaka 10, ambavyo vimezungumzia

mambo mbali mbali yanayofaa na yasiyofaa kuzungumzwa. Lakini kwa mtazamo wangu kuna jambo moja naona kama limesahauliwa kuingizwa.

Kwa hivyo, naomba kutoa pendekezo langu juu ya hilo au kama limo ama kuna kifungu ambacho kimo kitahusiana na suala hili, basi wakati atakapokuwa Mhe. Waziri kufanya majumuisho naomba nisaidiwe.

Kwa mfano, kifungu cha 59 (8) naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 59 (9) kinasema hivi:-

"(9) Ni marufuku kwa Mjumbe yeyote:-

(a) Kutumia lugha ya matusi na kashfa.

(b) Kutumia haki yake ya kusema kwa madhumuni ya kutaka kucheleweshe shughuli za Baraza. Vimeendelea vifungu vya (c) na (d)" …

Mhe. Spika, nadhani kuna kifungu ambacho kimekosekana na hili liliwahi kunitokea huko nyuma. Wakati Mhe. Mjumbe anapozungumza jambo ambalo pengine hana uhakika nalo na Waheshimiwa Wajumbe tukataka atupe uhakika juu ya lile jambo ambalo analizungumza. Sasa pengine anayoyazungumza si matusi wala si kashfa, lakini yalikuwa yanahitaji uthibitisho fulani, ili tukubaliane na yale anayoyazungumza.

Kwa kweli mimi sijaona hapo, Mhe. Spika kwa mujibu wa Kanuni hii mjumbe anayehitaji uthibitisho juu ya yale maneno yanayozungumzwa na mjumbe hutakiwa kutoa neno utaratibu na kumtaka Mhe. Mjumbe kuthibitisha maelezo yake na kama atathibitisha sawa kama hakuthibitisha aombe radhi. Kwa hivyo, hapo nimeona ni kimya.

Vile vile kuna vifungu kwenye kanuni hii vinavyozunguza juu ya adhabu ya watu wa aina hiyo au hatua za kuchukuliwa, hatua mbali mbali. Kwa hivyo, nataka ufafanuzi juu ya jambo hilo na kama halipo, basi niombe kifungu hicho kiingizwe katika Kanuni yetu Mhe. Spika.

Suala jengine la pili ambalo ningependa nalo nipendekeze liingizwe. Sehemu ya Nne ya Kanuni yetu imezungumzia suala zima la Utaratibu wa Shughuli za Baraza, humu zimeelezwa taratibu mbali mbali ambazo tutakuwa sisi tunazifuata kama Wajumbe na Kanuni ndio muongozo wetu.

Lakini kuanzia kifungu cha 35 hadi 42 kuna vifungu tofauti ambavyo vimezungumzia mambo yanayohusiana na maswali ambayo Mhe. Mjumbe atauliza na kufafanuliwa utaratibu mbali mbali ikiwa na pamoja na kuwasilisha swali siku 21 kabla ya kikao na mambo mengine na utaratibu wa kuuliza maswali.

Mhe. Spika, kuna kipengele kimoja ambacho ninapendekeza kiingizwe ambapo wenzetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wao nadhani kipo, lakini kwetu hakipo. Wakati pale ambapo Mhe. Mjumbe amewasilisha swali lake mapema kwa mujibu wa taratibu, lakini Mhe. Mwakilishi haelewi swali lake litajibiwa lini, yaani hatufahamu kitu, isipokuwa tunakuja asubuhi na kuona kwenye *Order Paper* kumbe leo swali langu linajibiwa.

Sasa kwa upande wa Waheshimiwa Mawaziri, wao tayari wameshapelekewa taarifa kwamba siku fulani swali linahusu wizara yako, kwa hiyo wanajitayarisha. Lakini Waheshimiwa Wajumbe wao hawana matayarisho juu ya maswali ambayo wameuliza.

Kwa hivyo, ninaomba Kanuni yetu ieleze kabisa kwamba mjumbe aliyeuliza swali basi na yeye apelekewe taarifa mapema kujua kuwa siku fulani swali lake litajibika kama anavyoelezwa Mhe. Waziri, ili na yeye ajiandae. Kwa sababu wakati mwengine anaweza kuwa na dharura muhimu na swali lake likaulizwa na Mjumbe mwengine kwa mujibu wa Kanuni, pengine alikuwa na swali la nyongeza atakuwa amelikosa.

Kwa maana hiyo, atakapopewa taarifa mapema kwamba swali lako namba kadhaa ulioulizia kitu fulani, Wizara fulani litajibiwa siku fulani. Kwa hiyo mwenyewe ataanza kujitayarisha, nadhani huu utakuwa ni utaratibu mzuri wa kuuliza maswali na kupata ufanisi zaidi katika maswali.

Mhe. Spika, nakushukuru sana *(Makofi)*.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia mawili matatu. Kwa kweli mimi ninayomapendekezo yangu ya kuongeza kwenye Kanuni likionekana linafaa, basi napenda kupendekeza masuala mawili au matatu.

Kwanza napendekeza wakati wa Kamati ya Baraza Zima, Spika anabadilika na kuwa Mwenyekiti, yaani anatoka kwenye kiti cha juu cha Spika anakuja chini, anakuwa Mwenyekiti wa kuongoza Kamati ya Baraza Zima.

Sasa ninapendekeza wakati ule wa Spika kubadilika kuwa Mwenyekiti kama wenzetu wanavyofanya, basi na yeye apate muda lile Joho la Uspika alivue

kidogo na kuja kukaa kwa ajili ya kuongoza kamati, na baadaye arudi avae Joho lake na aendelee kuwa Spika. Kwa sababu wenzetu ndivyo wanavyofanya kama inawezekana, basi na mimi napendekeza tuwe na utaratibu huo.

Wakati Spika anaondoka kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza Zima, basi Joho lile la Uspika, kwa sababu Joho ndilo linaloonesha kama ni Spika. Kwa hivyo, Joho alivue kwa muda na kuja kukaa na kuongoza Kamati ya Baraza Zima. Baadaye anaporudi kwenye kiti cha Spika atavaa Joho na kuendelea na Uspika kama kawaida.

Suala la pili, juzi tulipokuwa kwenye semina Mhe. Said Ali Mbarouk alipendekeza, Dua ibadilishwe *Heading* badala ya Dua ya Kuiombea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iwe Dua ya Kuiombea Nchi yetu ya Zanzibar. Kwa sababu ndani ya dua imekusanya mambo yote ya nchi yetu pamoja na serikali.

Kwa hivyo, *Heading* iwe Dua ya Kuiombea Nchi yetu ya Zanzibar na hili halikuzungumzwa, napenda kulikumbusha kama lina umuhimu tena ni nzuri zaidi, kwa sababu serikali na watu wake, pamoja na vilivyomo ndani ya nchi vyote vinakokotwa, vinakuwa ndani ya dua hiyo. Mhe. Spika, hili nalipendekeza kwa sababu lina uhumi tena ni zuri *(Makofi)*.

Mhe. Spika, suala jengine lazima sisi humu tuwe wakweli, wawazi na tumuogope Mwenyezi Mungu. Kwa sababu tujue tumo humu lakini iko siku tutarudi kwa Mwenyezi Mungu na tutaulizwa, hivi ni nani asijejua humu kama Wawakilishi sote ni Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar katika majimbo yetu?

Lakini nani asiyejua huku kama sisi Wawakilishi na tunaongozwa na chama chetu. Sasa mtu anaposema sisi upande huu tunaongozwa na chama pamoja na kufuata maamrisho ya chama tutakuja kuacha kiti wazi. Hivi nyinyi upande wa Chama Tawala hamuongozwi na chama, nani asiyeongozwa na chama? *(Makofi)*.

Kwa mfano, siku zote tunatoka, Wawakilishi wa upande wa CCM wabakie tuendelee, inaonyesha wazi kwamba mnakuwa mnapitisha msimamo wa chama. Kwa hivyo, na sisi msituone wabaya, kama tukipitisha msimamo wa chama, na nyinyi mnao msimamo wa chama. Kwa maana hiyo, lazima tuwe wakweli na wawazi na tujue iko siku tutarudi kwa Mwenyezi Mungu *(Kicheko/Makofi)*.

Baada ya hayo machache naunga mkono hoja.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza nataka nianzie kwenye ukurasa wa 17 wa marekebisho kama kawaida yangu kuna maneno yaliyokosewa, sasa nahofu kuwa yatakapopelekwa kwa ajili ya kuchapishwa vizuri yataandikwa kama yalivyo kwenye mabadiliko.

Mhe. Spika, kwenye marekebisho ya kifungu cha 116 (4) mstari mmoja kabla ya mwisho kuna neno majibu, hili sio majibu kwa mujibu, na sio kwa majibu, hili naomba lirekebishwe.

Pili kwenye marekebisho ya kifungu cha 117 (3) mstari wa mwanzo taarifa ya Kamati Teule, hapa imeandikwa itawasilisha kwenye Baraza, usahihi iwe itawasilishwa kwenye Baraza. Mhe. Spika, haya ni marekebisho madogo tu ambayo nilifikiri kuna haja ya kutajwa.

Mhe. Spika, mengi tunayajadili. Na kuyajadili kwetu ndiko kutakakopelekea tukawa na kitu kilichokizuri. Kuna suala liliulizwa hapa kuhusiana na utaratibu, lakini naomba nikumbushe kuwa kifungu cha utaratibu cha 63. kwa hivyo, kifungu cha 63 (1) na (2) vinaeleza kuhusu masuala ya utaratibu na kiko wazi kabisa na wala hakikujifisha. Kwa maana hiyo, yule Mhe. Mjumbe aliyeulizia kuhusu suala la utaratibu mtu anapokosea au kuhitaji ufafanuzi, nafikiri kifungu cha 63 hakina tatizo katika hili.

Lakini jambo hasa nililolukusudia kulizungumza ni kuwa sijui kama tumesahau au tunajipumbaza. Mhe. Spika, unapozungumza kuwa upande huu huko (Upinzani) haukubali kitu ni kujipumbaza. Kwa sababu ninakumbuka ikiwa wenzangu wamesahau miaka miwili mfululizo, Bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi tunanyanyua mikoni miwili kwa ajili ya kuikubali, niambiwe kama ni uongo! *(Makofi).*

Sasa mtu anaposema sisi tunakataa kila kitu si kweli. Isipokuwa tunaangalia hoja na tunapoona hoja hii inastahiki kunyanyuliwa mkono kukubaliwa basi tunaikubali. Mhe. Spika, napenda tukiona lile linalotendekana tukalisema na lile ambalo halitendeki tukalisema kuwa hili halitendeki.

Kwa hivyo, kuna haja ya Waheshimiwa Wajumbe kusikiliza vizuri wakazi wa michango. Kwa mfano, jana wakati nilipozungumza kuna wanafunzi wanaohitimu Vyuo vya Ufundi, lakini wanapokwenda mbele hawataki tena kuendelea kwenye Vyuo vya Ufundi.

Ah! hoja hiyo ilipingwa kwa kuambiwa Vyuo vipya vya Mkokotoni na Vitongoji, hivi kweli vyuo hivi tayari vimeshatoa wanafunzi wa kwenda vyuo vyengine. Mhe. Spika, nilivyozungumzia ni vyuo ambavyo vimetoa wanafunzi

wa kwenda vyuo vyengine kwa mfano Kengeja. Sasa hoja kama hizi lazima tuzipime na kuziangalia wakati tunapozungumza na wala tusizisukume tu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, sina mengi ya kuzunguza, zaidi hasa hoja yangu kubwa ilikuwa ni kuhusu haya marekebisho ya makosa yaliomo kwenye huu waraka wetu.

Ahsante sana Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, wakati Mhe. Mjumbe alipokuwa akichangia mada hii juu ya suala la utaratibu ambao nilitaka Mjumbe anieleze kwenye Kanuni kifungu cha 63 ambacho amekisema. Lakini kifungu cha 63 kilichokuwemo hakizungumzi hilo nililolizungumza mimi. Kwa sababu kifungu cha 63 Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 63 (1) kinasema hivi:-

> "Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu, lakini Mjumbe huyo anapofanya hivyo itabidi ataje Kanuni ya Baraza …"

Mhe. Spika, nilichozungumza mimi kwamba, Kanuni ya Baraza ndiyo iliyokosekana hapa, yaani imekosekana kanuni. Kwa hivyo, hata nikisema kuhusu utaratibu Kanuni humu iko *silence*. Kwa maana hiyo, kiangaliwe kicho kifungu cha *silence* juu ya mtu wa aina hiyo anayezungumzia hivyo, nadhani nimeeleweka. Kutokana na hali hiyo ningeomba Mhe. Mjumbe mara nyingi aachie wenyewe wahusiku kujibu *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Kanuni za Baraza letu tukufu.

Kwa mujibu wa utaratibu, Waheshimiwa Mawaziri huwa tunawauliza maswali ambayo huitwa maswali mama, lakini kuna maswali ya nyongeza. Mhe. Spika, wapo Mawaziri majibu yao ya maswali ya nyongeza hayafanani na lile swali la nyongeza aliloulizwa.

Kwa kweli huishia pale pale, maana yake yeye akishakujibu, basi hakuna chengine chochote kinachoendelea kwa yule aliyeuliza swali ameshakaa kitako na waziri aliyejibu swali la nyongeza anaondoka kwenye membari na kwenda kukaa kitako. Mhe. Spika, swali kama yale hakuna aliyefaidika na zaidi yule aliyeuliza. Kwa sababu hakuna jibu ambalo linafanana na swali lile.

Mhe. Spika, kwa kweli hawaishii hapo Mawaziri au Manaibu Waziri hao, wanaeleza kwamba swali hili majibu yake nitaleta kwa maandishi. Kwa sababu mimi nimeshauliza na kujibuwa hivyo mara nne na nilipata majibu ya maandishi mara moja.

Kwa hivyo, ninapendekeza kwamba katika ahadi hizi za Mawaziri au Manaibu Waziri kwa mswali yale ya kujibu kwa maandishi, basi Kanuni ingetaja, yaani ingepewa muda kabisa kama ni wiki moja au mbili lile jawabu liwe limepatikana. Lakini haiwezekani kwa sababu ukisema nitatoa kwa maandishi ikafika siku tano au wiki tano na hata mwaka bado atatoa. Mhe. Spika, inafika mpaka Baraza hili kumalizika hajatoa. Sasa huwezi kusema kwamba *he was correct or not.*

Kutokana na hali hiyo, napendekeza Kanuni ingetoa kifungu kidogo na kuchomekwa sehemu ambayo inayofanana. Kwa maana hiyo, Mawaziri au Manaibu Waziri wakapewa muda maalum, kwamba jibu la maandishi liwe limefika tena si kwa yule muulizaji peke yake.

Kwa sababu tukiuliza maswali hapa si kama wanajali, lile nikipewa au akipewa Mhe. Mjumbe mwengine yoyote kwamba ni lake mwenyewe lazima lisambazwe kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kuwa hili ndilo jawabu ambalo liahidiwa kwa maandishi. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, kuhusu Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Baraza hili. Miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ni Wenyeviti wa Kamati za Baraza hili. Kwa kweli mimi sijawahi kuhudhuria kwa sababu sina ***portfolio*** yoyote ya kuingia humu. Isipokuwa naamini wakati Wenyeviti wa Kamati wamo, masuala ya kamati nayo huwa yanahojiwa, na hizo ndizo fikra zangu. Kwa sababu Wenyeviti wa Kamati ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, basi *logical* masuala ya kamati zao kama italazimika huwa yanaulizwa au yanajadiliwa.

Lakini Kanuni zinaeleza Mwenyekiti wa Kamati, ninapendekeza kwa sababu kuna wakati Mwenyekiti wa Kamati hahudhurii kwa sababu zozote zile kama vile ugonjwa na wala si kikao kimoja au viwili na hata vitatu. Sasa huwa ninajiuliza inapotokea Mwenyekiti wa Kamati fulani hajahudhuria kikao cha Kamati ya Uongozi kwa kipindi fulani, hivyo kamati ile inawasilishwa na nani na shughuli zake zinajulikana vipi katika Kamati ya Uongozi?

Mhe. Spika, napendekeza Makamo Wenyeweviti wasiwe Wajumbe wa kamati, lakini waweze kualikwa kama Kamati ya Uongozi inataka kujua habari za

Kamati ile na Mwenyekiti wake anajulikana kuwa hayo ama yuko safarini au mgonjwa na hata vyengine vyovyote. Hilo ni pendekezo langu la pili *(Makofi)*.

Mhe. Spika, Baraza hili ukisema ni Baraza la Wawakilishi wa *CUF* na CCM utasema tu, lakini sema ni Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wanaowakilisha Baraza hili ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar. Kwa kweli sote ni mashahidi na wananchi wa Zanzibar ndio mashahidi zaidi *(Makofi)*.

Kwa mfano, zilipokuja hoja za Zanzibar nchi na ile hoja ya mafuta. Kwa sababu hizi ni hoja mbili ambazo zimeweka historia katika Baraza hili, namna ambavyo pande hizi mbili tulivyokuwa Wazalendo na kusahau yote ambayo tunayo na wananchi wa Zanzibar wakasema *yes, it can be done, we can deliver (Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya Baraza hili kumbukumbu zangu nafahamu hivyo, kwamba hoja iliyoletwa na serikali hapa ya mafuta, tulijidajili na hatimaye ikaungwa mkono kwa asilimia mia moja na Wajumbe wote wa Baraza hili.

Sasa inanishangaza sana kusikia kwamba upande huu wa Chama hiki cha *CUF* watakapoweza kupata nafasi ama ya Uspika au Naibu Spika ama Wenyekiti na sasa Wenyeviti wanapendekezwa kuwa wawili, basi hawa wote wawe wanatoka upande mmoja, kwa sababu ya demokrasia. Lakini demokrasia haina uzalendo, umoja na watu kuwa waonekane kuwa kweli hawa wenzetu wamesogea hatua moja mbele na wengine wanasogeleana *(Makofi)*.

Mhe. Spika, tusione leo hakuna fundi kama Mwenyezi Mungu, yaani uwezo wake ni mkubwa tena bila ya mipaka. Kwa hivyo, inaweza kutokezea kabisa na wala si maajabu kwamba huko kukawa huku na huku kukawa huko, yaani upande wa chama tawala ukabadilika na kuwa upande wa upizani. Hivi mnadhani sisi tutafanya hivyo mnavyofanya nyinyi, kwa kweli ni *never*, kwa sababu tukimchagua upande huu chama chake kitamwambia asende kwa hiyo kiti kitakuwa wazi.

Kwa kweli Spika mwenyewe ni CCM yaani Mjumbe wa Halmashauri Kuu, Naibu Spika CCM, Mwenyekiti CCM. Hivi haiwezekani wote ikawa hawapo? Kwani hawa si binadam? Wahaumwi au hawasafiri? Sasa haijatokea, lakini inapotokea hivyo tunafanye nini? Kwa hivyo, msidhani kama kuna haja ya kuleta hoja kama hizi kwamba ikitokea huko nyinyi mtakuwa hivi na vile *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nafikiri twende katika suala la uzalendo na lionekane Baraza hili tofauti zinaanzwa kufutwa. Lakini kila siku tofauti zinafutwa na halafu

zinaandikwa nyengine. Kwa hiyo, sidhani hoja kama hizi zikionekana zinazungumzwa kwenye baraza watu wanatuonaje ambao tunaowawakilishi huko *(Makofi).*

Baada ya hayo machache nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kutoa ufafanuzi kwa masuala au michango waliyoitoa kuhusiana na marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Mhe. Waziri Kivuli wa Afisi ya Waziri Kiongozi ametoa maelezo na mimi kunipatia *copy* za maandishi. Vile vile napenda kuwatambua na wengine waliochangia katika marekebisho haya ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ambao kwa jumla walikuwa ni Waheshimiwa Wajumbe 10 ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheri na Utawala);
2. Mhe. Zahra Ali Hamad (Kny: Mhe. Abubakar Khamis Bakary Waziri Kivuli wa Afisi ya Waziri Kiongozi);
3. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi;
4. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira;
5. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja;
6. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi;
7. Mhe. Salmin Awadh Salmin;
8. Mhe. Subeit Khamis Faki;
9. Mhe. Mohamed Ali Salim;
10. Mhe. Hamad Masoud Hamad
11. Mhe. Zakiya Omar Juma na
12. Mhe. Said Ali Mbarouk

Kwa hivyo, hao ni wajumbe ambao walichangia marekebisho haya ya kanuni.

Mhe. Spika, kama nilivyosema katika ripoti yangu kwamba nimempongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa sababu yale mapendekezo mengi ambayo waliyoyapendekeza mengi yao tuliyachukua na yamo katika marekebisho ya kanuni ambayo tuliyoileta. Kwa hivyo, mimi sitaki niongeze lolote isipokuwa kama nilivyosema mwanzo nilikuwa nawashukuru kwamba wametusaidia sana yale ambayo sisi hatukuyaona wao wamekuja kutushauri.

Vile vile nikija kwa Mhe. Zahra ambaye yeye ndio ameongoza kambi ya upinzani, amekiri kwamba katika yale maoni waliyoyatoa kwenye kamati ni

kwamba yamechukuliwa. Pia amepongeza kuingizwa wimbo wa taifa wa Zanzibar, hili ni jambo ambalo litakalotusaidia.

Mhe. Spika, pia Mhe. Zahra alihoji kwamba je, baada ya kukubali huu wimbo wa taifa kuimbwa hatutoitwa na Kamati ya Mhe. Ali Hassan Mwinyi. Mhe. Spika, kimsingi najua Mhe. Zahra yumo katika utani, lakini utani wake huu ameutia kwenye maandishi. Kimsingi haya ni maamuzi kwa sababu hapa tunarekebisha Kanuni za Baraza na Baraza lina maamuzi yake. Kwa hivyo, suala lolote ambalo tunaliamua tukiliona na maslahi ya taifa basi sote tunakuwa kitu kimoja na tunaunga mkono. Katika yale mambo ya kimsingi mara nyingi jambo lolote unapolifanya lazima uangalie na nidhamu ya chama chako na hili halina ubishi, kwani kila mmoja analijua hilo.

Mhe. Spika, ndio maana hapa kunakuwa na wanadhimu wawili, Mnadhimu wa Chama Tawala na Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani. Katika masuala haya nadhani wanadhimu wanaangalia zaidi maslahi ya vyama vyao na maslahi ya taifa. Kwa hivyo, hili lisiwatie wasi wasi kwamba hii kamati haitotuhoji katika hili.

Mhe. Spika, ni kwamba nataka niwatoe wasi wasi kwamba ile kamati sisi tumeifurahia sana, ile kamati ni tofauti na watu walivyokuwa wanafikiria. Labda nitoe siri ya kikao kwamba tumependekeza kuwa ile kamati iendelee kwa sababu imetufurahisha, na hili tunalizungumza wazi wazi kuwa tumewaambiwa tunakushukuruni sana kwa kuja kutusikiliza na kutusikia nini tunachokisema na kama kuna ujumbe basi mtupelekee, lakini tunapendekeza muendelee kuwepo mtatusaidia sana katika mustakabal wa taifa letu na muungano wetu wa Tanzania.

Mhe. Spika, hili mimi nafikiri tusiwe na wasi wasi nalo kwa sababu tumeshafanya mambo mengi tu katika marekebisho ya kanuni zetu na katiba na hakuna hoja yoyote ambayo iliyokuwa nzito ikatuletea mtafaruku. Nadhani kutokana na wajumbe walivyochangia hata katika ile semina yetu sikuona mjumbe yeyote kupinga kuwepo kwa wimbo wa taifa. Kwa hivyo, wimbo wa taifa tukijaaliwa utakuwepo na kama tulivyosema kanuni hizi kama mtazikubali basi katika kikao kijacho tutaanza kukitekeleza. Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kuanzia leo tuanze kujifundisha wimbo wa taifa wa Zanzibar ili tukija hapa tuwe tunauimba vizuri.

Mhe. Spika, unapoimba wimbo wa taifa kwa kiasi fulani mwili wako unakusisimka yaani ule uzalendo hapo ndio unakujia. Mhe. Spika, hili nafikiri kwa pande zote mbili tumekubaliana na sitegemei kama kuna atakayepinga, na atakayepinga itabidi tutamuangalia kwa macho matano, lakini nawaambia wajumbe wawe huru tutakapopitisha mambo haya.

Mhe. Spika, nikiendelea Mhe. Machano Othman Said kuwa je wimbo huu utaimbwa *live* au italetwa bendi ya polisi au waheshimiwa wenyewe wataimba. Mhe. Spika, mapendekezo yetu ni kwamba tutarikodi *CD* ambayo kila Baraza tutakuwa tunaifungua, lakini na wajumbe wenyewe watatakiwa waimbe kwa midomo yao. Ile *CD* itakuwa inatuongoza tu lakini wajumbe wenyewe watakuwa wanaimba huo wimbo.

Mhe. Spika, Mhe. Machano alitupongeza kwa marekebisho ya kanuni kabla ya marekebisho haya ni kwamba kikao kinapoahirishwa kwa kumaliza shughuli zetu tulizozipanga ni kuwa Mhe. Spika anamuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kuliahirisha Baraza. Inabidi Waziri anasimama kumuomba Mhe. Spika aliahirishe Baraza, kwa hivyo Mhe. Spika anawaomba wajumbe kwamba nani anaunga mkono.

Kwa hivyo, tuchukulie kwa kanuni yetu sasa hivi kama kuna siku Mhe. Spika, baada ya kuombwa na Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi aliahirishe Baraza wajumbe wote wakakataa na shughuli tulizozipanga itakuwa tumemaliza je, tutafanya nini? Itabidi sasa tutizamane hapa kwani itakuwa hakuna shughuli ya kufanya kwa sababu wajumbe kwa kuwa wako huru na hili Baraza limo chini ya utawala wao jambo lolote akiliamuru Spika wao wakilipinga itabidi Spika abakie juu ya kiti na wajumbe wabakie kwenye meza zao wakitizamana.

Mhe. Spika, kama siku wajumbe watakaotufanyia vituko hapa nafikiri magazeti yote siku hiyo wangeliandika Baraza la Wawakilishi hawajui nini wanachokifanya. Kwa hivyo, baada ya kutanabahi ndio tumeleta haya marekebisho na tunashukuru wajumbe wengi wameonesha nia ya kuwa Spika awe na uhuru tunapomaliza shughuli zetu atamke kwamba tunaahirisha Baraza.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Machano alihoji katika kifungu cha 104 kwamba mawaziri wanatakiwa wawe wanashiriki katika kamati. Mhe. Spika, hili Kamati ya Uongozi iliagiza kipindi kirefu, lakini baada ya kuona kuna baadhi ya mawaziri hatuwajibiki vizuri kamati zinapokwenda tunajifanya tuna shughuli nyingi ndio wajumbe wameona waliingize ndani ya kanuni ili mawaziri wawajibike moja kwa moja kama katiba inavyosema ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, hili tutalitolea toleo pamoja na kwamba tutapitisha katika kanuni lakini afisi yangu itatoa toleo kwa mawaziri wote kamati zinapokwenda katika mawizara yao wahakikishe wanashiriki. Kwa mfano, kama wizara itakuwa na Naibu Waziri ikiwa waziri ana shughuli nyingi basi Naibu Waziri anaweza akajumuika na wajumbe ili kujiridhisha kwa kila masuala ambao yatakayoulizwa waziri aweze kutoa ufafanuzi wa kutosha. Hii itatupunguzia masuala mengi pale zinapokuja ripoti za kamati kwa sababu

kama masuala yatakuwa yameshajibiwa kule, basi ripoti zetu zitakwenda vizuri sana.

Mhe. Spika, pia aliuliza kwa nini mawaziri wasiwe na haki ya kupiga kura.

Mhe. Spika, mawaziri ni serikali, wajumbe wa kamati ni wananchi kwa hivyo wananchi wanapojenga hoja katika masuala yao wanatakiwa wawe huru zaidi, ndio maana pale mawaziri wao watatakiwa zaidi wajibu masuala hayo. Lakini katika masuala ya kupiga kura mawaziri hawatoruhusiwa kupiga kura kwa sababu hawatakiwi waingilie moja kwa moja shughuli za kamati, wao watatakiwa zaidi watoe ufafanuzi. Nategemea kama watatoa ufafanuzi mzuri nafikiri kutakuwa hakuna haja ya wajumbe kufikia pahala kupiga kura. Kwa sababu waheshimiwa wanapokwenda serikalini wanataka kujua kile ambacho walichokipitisha, vipi kimetumika, vipi utekelezaji wa shughuli hiyo.

Ndio maana sasa hivi kuna utaratibu uliokuja kwamba watu wanataka wajue *value for money* ile fedha iliyoidhinishwa imetumika vipi na je vile ilivyotumika imetumika katika kiwango ambacho kinastahili. Kwa hivyo, kama tutakuwa na jawabu nzuri wajumbe watakuwa hawana haja tena kuanza kutupigia kura, watakapotupigia kura wataonesha kwamba hawakuridhika na ule utekelezaji wetu. Kwa hivyo, hili Mhe. Machano ufafanuzi wake ndio kama huo.

Mhe. Spika, pia mheshimiwa amependekeza kwamba wanadhimu wa vyama tusiwaingize katika Kamati ya Uongozi, hili limerejewa na waheshimiwa wengine. Mimi niseme kwa kiasi fulani nakubaliana na hoja za wajumbe kwamba wenyeviti watakuwa wanawakilisha zile kamati zao katika Kamati ya Uongozi na kule zaidi kunazingatiwa masuala ya utendaji wa kazi za Baraza na namna ya maslahi na mambo mengine ya Baraza nadhani masuala ya vyama yanakuwa hayahusiki sana.

Kwa hivyo, hili Mhe. Spika, nakiri na yale mapendekezo ambayo tumeyapendekeza mwanzo ya kuwa wanadhimu waingizwe nitakubaliana na hoja za waheshimiwa kwamba wanadhimu tuwapumzishe. Lakini nitawaomba viongozi au wajumbe wa vyama vyote viwili katika kuwapa heshima basi wanadhimu wetu tujaribuni kuwapa hizi nafasi ambazo zitakazoweza kuwaingiza moja kwa moja katika Kamati ya Uongozi ya Baraza.

Mhe. Spika, katika Tume ya Bajeti Mhe. Machano alieleza kwamba anaunga mkono ianishwe sasa hivi moja kwa moja katika kanuni kuwa mjumbe yeyote anapokuwa ni mjumbe wa kamati au wa Tume ya Bajeti anapopata nafasi ya Waziri, Naibu Waziri au Mkuu wa Mkoa atoke moja kwa moja. Ni kweli kwa sababu kama sasa hivi ile Tume yetu ya Bajeti nafikiri kuna wajumbe wawili

wote wamepata nafasi za waziri ina maana sasa ule uwakilishi moja kwa moja wa wajumbe katika tume yetu unatawaliwa na serikali zaidi. Mhe. Spika, ni kwamba chombo hiki kinatakiwa zaidi kitawaliwe na wajumbe wenyewe.

Hilo nafikiri kwa sasa hivi kweli yapo mapungufu na kweli wakati mwengine tunapotakiwa kuingia katika Kikao cha Tume ya Bajeti mara nyengine tuko katika majukumu ya wizara huku ina maana ule uwakilishi unakuwa unakosekana. Nadhani baada ya kuikubali kanuni hii nitaomba kanuni hii tuikubali kwa pande zote mbili kwa sababu kama hatujaikubali inamaana bado kazi zetu zitakuwa zinaendelea kudhorota. Kwa hivyo, tukiikubali hii moja kwa moja wale wajumbe wawili ambao kwa sasa hivi wamepata nafasi ya uwaziri basi moja kwa moja ule ukomo wao wa kuwa wajumbe wa Tume ya Bajeti uwe umemaliza ili tutakapoingia katika kikao kijacho tuweze kufanya uchaguzi kwa wale wajumbe wengine waingie katika Tume ya Bajeti.

Mhe. Spika, Mhe. Machano pia aliuliza uchaguzi wake utakuwa lini. Mimi nadhani baada ya kupitishwa hii kanuni itabidi tutatoa toleo kwamba wale wajumbe ambao nafasi zao sasa hivi ziko wazi, tutatoa barua kwa wajumbe hatutosubiri katika kikao watapekewa huko huko ili mtu atakayetaka kujaza ile nafasi ajiandae mapema ili kuweza kufanya kampeni.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Machano kwa sababu alisema wale wajumbe wa Tume ya Bajeti mmoja wapo alikuwa ni yeye. Alisema kwa nini wao ni wajumbe halali lakini hawalipwi posho na kamati nyengine zote huwa wanalipwa posho. Nikasema swahibu wangu inaonesha atakuwa mtu wa peponi kwa sababu hii nafasi anaiacha ndio anaiombea posho, pale alipokuwepo hakuomba posho alikuwa anafanya kazi kizalendo.

Mhe. Spika, ufafanuzi wake ni kwamba wale ambao wanalipwa posho mara nyingi wanakuwa wanashikilia nyadhifa tofauti. Lakini Baraza letu litajaribu kuangalia mchakato wetu wa bajeti kwa sababu wakati mwengine tukilipana maposho mengi na uwezo wa kuendesha shughuli zetu za Baraza zitakuwa zinapungua. Mhe. Spika, lakini ni hoja ya msingi kwa sababu inawezekana kwamba mjumbe aliyechaguliwa ni mjumbe wa Tume ya Bajeti.

Kwa mfano, kikao kipo Unguja na yeye yuko Pemba kweli utamwambia ashiriki katika kikao wakati hukumpa nauli wala posho ataishi vipi katika mazingira hayo. Kwa kweli ni hoja ya msingi sana hivyo tutajaribu kuangalia ili na wao hawa wajumbe waweze kulipwa posho. Kwa sababu posho tofauti na watu wengine wanavyofikiria kama sasa hivi kuna malumbano makubwa huko, wenzetu wamewachokoza TAKUKURU sasa hivi imewageukia wao.

Mhe. Spika, hoja ya posho sasa hivi inatafsiriwa vyengine ni kwamba posho ni ya kumfanya yule mjumbe aweze kufanya kazi bila ya matatizo. Haiwezekani unamchukua mjumbe huko unamleta hapa anaanza kwenda kupiga virungu, hiyo itakuwa haipendezi. Mhe. Spika, chombo hiki kina heshima yake inatakiwa mjumbe anapotumwa kazi awezeshwe na ndio maana akaitwa mheshimiwa, hata katika sehemu anazokwenda waheshimiwa wanatakiwa wakae nafasi za mbele. Kwa hivyo, mapendekezo yake Mhe. Machano tunayakubali kwamba hawa wajumbe wapya watakaoingia baada ya marekebisho haya ya kanuni watapata angalau pesa ya kujikimu.

Mhe. Spika, nikiendelea na michango ya wajumbe vile vile Mhe. Machano aliunga mkono suala la marekebisho. Kweli tulikuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunazuiwa kungia na simu na pia simu hizo zisilie ndani ya ukumbi. Mhe. Spika, ni kwamba hatukuweka utaratibu juu ya wale wageni wetu lakini tuliweka matangazo pale mlangoni wanapoingia kwamba simu zao wazifunge ili wasije wakakutwa na adhabu. Kwa sababu mjumbe yeye anaweza akakatwa posho je, yule mualikwa atakatwa nini. Wale wageni wao itabidi wapelekwe rumande lakini itakuwa haipendezi mtu ukimpeleka rumande basi haji tena hapa. Kwa kifungu ni kwamba tunarekebisha hizi kanuni lakini wale wageni wetu ni vizuri wakaelekezwa mapema masharti ya humu ndani.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma yeye amepongeza kwamba wamekubali wawe na wimbo wa taifa na alisema kwamba Zanzibar ni nchi, Zanzibar ina Rais wake, ina bajeti yake, ina Baraza la Wawakilishi, Mahakama, wimbo wa taifa na mambo mengine mengi. Kwa hivyo, alisisitiza kwamba hili ni wazo zuri limekuja na limekuja kwa wakati muafaka. Mhe. Spika, kwa sababu wakati mwengine tunakuwa hatujisikii vizuri, wenzetu Bunge la Jamhuri wanapofungua unaimbwa wimbo wa taifa, hapo kila mmoja anang'ang'anaa na waheshimiwa wanaigiza. Kwa hivyo, tukasema na sisi kwa nini tuendelee kukaa nyuma basi tukasema madhali Zanzibar ina wimbo wake basi tuimbe wimbo wetu wa taifa.

Mhe. Spika, pia Mhe. Zakiya alipendekeza kuwa Spika akiwa ametoka chama kimoja basi Naibu Spika atoke chama chengine au wenyeviti. Mhe. Spika, suala hili wajumbe wameshaliogelea na mimi nitataka nizungumze kitu kimoja. Ni kwamba Mhe. Spika anapokuwa katika kiti hiki kwanza kuna taratibu za uongozi na uongozi wowote ukishakukabidhiwa basi kuna miko yake unatakiwa uifuate. Kwa hivyo, kiti hiki kama akiwa Spika, Naibu Spika au Mwenyekiti basi lile joho lake la chama anatakiwa analivua anakalia kiti cha Spika. Kwa sababu anapopigiwa kura hapigiwi na chama chake anapigiwa na wajumbe wote, na sisi hili tumethibitisha kwa sababu katika kura tulizozipiga upande wa upinzani walimpigia na chama tawala walimpigia na ndio maana akaweza kuwa Spika wetu.

Mhe. Spika, hapo tukitaka kupeleka kwa utashi wa chama itabidi sasa amsikilize mnadhimu anasemaje, akimwambia leo inama basi itabidi ainame, akimwambia inuka basi itabidi ainuke. Pia mnadhimu akimwambia leo tusiingie tutakuja hapa kiti kitupu, na kitu hiki kwa bahati mbaya hakikai kitupu, kikikaa kitupu kiti hiki basi atakaa shetani itakuwa hatuna Baraza. Kwa hivyo, mimi naomba sana tuendelee na utamaduni wetu ambao tumejijengea siku zote. Mhe. Spika, kuna wale wanaosema kwamba waheshimiwa wana migongano ni kwamba sisi hatuna migongano. Sisi waheshimiwa tunafanya kazi kwa pamoja na tunashirikiana wala hatuna matatizo yoyote. Kwa hivyo, ndio maana tukasema viongozi wetu wanachaguliwa na pande zote mbili.

Mhe. Spika, kuna mambo sisi wenyewe tunataka tujenge upendo tusisubiri kila kitu kiingizwe kwenye kanuni. Kwa sababu kila kitu tukiingiza kwenye kanuni wakati mwengine ile demokrasia yetu itakuwa inalazimishwa mambo ambayo hayawezekani. Mimi nitatoa mfano mdogo tu. Hapa tulifanya uchaguzi wa wabunge kupitia Baraza la Wawakilishi, tuna nafasi tano za wabunge wanaingia Bungeni. Kwa kweli hili halimo ndani ya kanuni kwamba lazima wengine watoke chama cha upinzani na wengine watoke chama tawala. Lakini tumeona kuwa tunawapeleka kule wenzetu ili yale mawazo yetu yaweze kuwa pamoja tumelifanya hili na wala hatukulazimishana.

Kwa hivyo, mimi naona kuna masuala mengine tukijenga ule ushirikiano basi tunaweza kuyafanya bila ya kulazimishwa baadhi ya kanuni zetu. Mhe. Spika, hiki chombo mara nyingi mambo ya humu ndani jambo lolote linaloitwa la Baraza basi utashi wa kisiasa unakuwa unakaa pembeni. Kwa sababu tukifanya kazi kwa utashi wa kisiasa sana tutawaumiza wananchi wetu ambao wametuleta hapa. Mhe. Spika, mimi nasema tuendelee kujenga imani nzuri ndio tutaweza kushirikiana vizuri kama tunavyoshirikiana katika mambo mengine.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ajenda nafikiri ameliunga mkono kwamba ni vizuri katika nafasi hizi mapendekezo ni kwamba sasa hivi tuna mwenyekiti mmoja tukiwa na wenyeviti wawili kukawa kuna masuala ya ajenda tukayazingatia. Aidha wawe wanawake au wanaume, lakini hapo hapo katika marekebisho yetu ya kanuni tulisema ikiwa watajaza wanawake watupu basi haitolazimishwa kwamba uchaguzi usifanyike kwa kuwa wanaume hawakujaa. Au wakijaza wanaume watupu uchaguzi usifanyike kwa kuwa wanaume hawakuja kwa sababu ni demokrasia. Lakini kama atatokezea mwanamke basi huyo katika mchujo lazima jina lake liwemo na inabidi wajumbe washawishike kwamba katika kutekeleza haya masuala ya ajenda basi aungwe mkono.

Mhe. Spika, tunategemea pengine kuanzia vikao vyetu vya Januari inawezekana tukaja kumkuta mwa mama pale amepiga joho kwa kusimamia Baraza. Kwa hivyo, nafikiri kina mama changamoto hii kuanzia sasa hivi muanze kampeni kwa ajili ya kuchaguliwa hiyo nafasi. Lakini tunawaomba wale ambao watakaojaza hizi nafasi wajue kwamba hiki kiti ni kizito, isije ikafika pahala ukaja ukakikimbia kiti. Nafasi hiyo ni nzito ni nafasi ambayo inatakiwa kidogo ujue masuala ya sheria na kanuni iwe ndio chakula chako, usije ukakaa pale unapigiwa buti unaanza kumwita katibu wake njoo unisaidie.

Mhe. Spika, nikiendelea na michango ya Mhe. Zakiya namwambia kwamba asiogope sana ukiristo kila mtu atafuata dini yake. Lakini hivi vivazi vina tamaduni zinakuwa kama zinaendana. Kwa mfano, ukiangalia wanafunzi wa vyuo vikuu wanapokuwa katika mahafali yao ukiangalia vile vivazi vyao vinakuwa vinalingana na baadhi ya madhehebu, lakini kuna wengine ni waislamu nao wanavaa.

Kwa hivyo, mimi naona kuna baadhi ya mambo tusiyachanganye sana tukiyachanganya sana baadhi ya mambo hasa masuala ya dini yanakuwa very *sensitive*. Pia katika chombo chetu hiki tunatakiwa tuzungumzie suala la umoja, Zanzibar tunajua karibu asilimia kubwa ni waislamu na asilimia ndogo sana ni wageni. Kwa hivyo, tunatakiwa tuwaheshimu kama tunavyowaheshimu hawa waislamu hapo ndipo tutakapoonekana kwamba hiki chombo kinafuata katiba, utawala bora na demokrasia. Mhe. Spika, mimi nafikiri masuala haya tusiyaingize sana katika muelekeo wa kidini utakuja kutuharibia mwenendo wetu mzuri ambao tunakwenda nao sasa hivi.

Mhe. Spika, Mhe. Khatib Suleiman Bakari na yeye alitoa mchango wake na kutoa indhari kwamba tunapofanya maamuzi katika chombo chetu hiki tuangalie na utamaduni tulioujenga katika nchi yetu hasa masuala yetu ya upinzani ndani ya Baraza kiti kisije kukaa kitu. Nafikiri hili nimeshalitolea ufafanuzi.

Vile vile namshukuru kwamba mwenzetu amesoma Kijerumani ametutolea ufafanuzi wa shule na skuli. Kwa hivyo, mimi nafikiri yule aliyesema shule atakuwa hakukosea na aliyesema skuli vile vile hakukosea.

Mhe. Spika, nikiendelea na hoja za waheshimiwa pia Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim amesema kwamba ile hoja ya mjumbe kucheleweshe Baraza. Mimi nafikiri suala hili tayari limo ndani ya kanuni zetu na katika hayo marekebisho yatakayokuja nadhani litajionesha wazi wazi. Kama tulivyosema kwamba hii kanuni ambayo tunaisoma sasa hivi ina baadhi ya mapungufu mengi, haya mapungufu ambayo yamejitokeza huku ndio haya marekebisho ambayo tunayafanya sasa hivi. Kwa hivyo, nadhamu Mhe. Mustafa hili suala asiwe na

wasi wasi nalo katika marekebisho haya tumelizingatia na litaonesha wazi wazi.

Vile vile Mhe. Spika, suala la *financial bill* Mhe. Said Ali Mbarouk hili amelizungumza na kimsingi liliwahi kujitokeza kama sikosei katika vikao vya Bajeti vya mwezi Julai. Hili lilizungumzwa nafikiri hii hoja Mhe. Said alijaribu kuieleza na leo ameikumbushia tena. Kwa hivyo, suala hili kimsingi Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha alilikubali na tumo katika kulifanyia utaratibu. Kwa hivyo, Mhe. Said nadhani tuwe wastahamilivu, tutapokuja katika kikao cha bajeti cha Julai, nadhani kutakuwa na mabadiliko yatakayokuwa yamejitokeza.

Kama tulivyosema kwamba sisi kazi yetu kuwasikiliza Waheshimiwa Wawakilishi wanasema nini kwa sababu wao ndio watumishi wa wananchi na wanaiambia serikali na yale yote mnayotwambia tunayarikodi na tunajaribu kuyafanyia kazi. Kwa hivyo, hakuna jambo linalosemwa hapa likaachwa hapa hapa, mabadiliko mengi yanayofanyika basi yanakuja kwa hoja za wajumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na yeye vile vile alitoa mchango wake na alisisitiza, kama nilivyosema kwamba alirejea kuwa kuna baadhi ya maeneo tusijaribu kuangalia utashi wa vyama hasa katika suala la uchaguzi wa Spika na Wanadhimu kuwaingiza katika Kamati ya Uongozi. Lakini vile vile kama alivyosema kuwa unapoongeza wajumbe katika hizi kamati zetu basi unaongeza matumizi ya serikali. Sisi kama kawaida tunavyotakiwa kwamba serikali tujitahidi kupunguza matumizi ili fedha zile ziingizwe katika shughuli za kiutendaji.

Kwa hivyo, kama nilivyosema mwanzo kuwa kuna baadhi ya haya maoni ambayo tumeyaletea marekebisho basi tunakubali kuwa wale wanadhimu tunakiri kwamba hatutowaingiza tena katika Kamati ya Uongozi, lakini katika uchaguzi wa Spika tutaomba watu wajenge yale mahusiano mema ili mtu yeyote aonekane kwamba anaweza akapewa hii nafasi ya Unadhimu, Spika au Mwenyekiti wa Baraza.

Mhe. Spika, pia Mhe. Salmin Awadh na yeye ametoa maoni yake na pia alisema zaidi katika kifungu cha 59 kwa yale mambo yanayofaa na yasiofaa. Kwa hivyo, alipendekeza nyongeza na kama nilivyosema kwamba, katika haya marekebisho tunayoyafanya katika *version* hii ya sasa hivi hili suala halimo. Lakini kupitia tangazo la serikali rasmi lililotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali basi vifungu vyote hivyo vitaonekana katika hili chapisho jipya litakalokuja. Tutajitahidi basi hayo marekebisho ya hii kanuni tutaifanya kwa

haraka haraka ili ije mapema, kwa sababu tukishafanya marekebisho haya basi zile kanuni za mwanzo zitakuwa haziwezi kufanya kazi. Kwa sababu mtu atakuja kunukuu kifungu na kupiga buti hapa lakini kifungu anachokihoji kumbe kitakuwa kimeshafanyiwa marekebisho. Kwa hivyo, hili Mhe. Salmin tumelichukua tumelifanyia kazi nafikiri katika marekebisho yetu litakuja kuonekana.

Vile vile suala la mjumbe kuthibitisha kauli yake. Mhe. Salmin alimrejea Mhe. Moh'd Ali Salim kwa kufanya marekebisho kwamba yale aliyoyakusudia yeye sio yale aliyoyazungumza yeye. Hii kanuni ya kusema kwamba mjumbe anaweza akazuia kifungu lakini bila ya kutaja kanuni. Hili kweli ni kosa kwa sababu unapozuia kifungu inabidi lazima utaje na ile kanuni inayotakiwa ufafanuzi. Kwa hivyo, hili vile vile Mhe. Spika, tumelizingatia nadhani katika haya marekebisho basi yatakuja kuonekana wazi wazi.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Salmin alizungumzia katika kifungu cha 32 cha kanuni mpaka 42 kinaelezea utaratibu wa kuuliza maswali na ule muda tuliouweka katika suala zima la kuuliza maswali.

Mhe. Spika, mjumbe anavyotakiwa aulize swali zisipungue siku 21 kabla ya swali lile kuja kuletwa hapa ili waziri apate kujibu kwa ufasaha. Kwa sababu unapompelekea waziri swali ghafla waziri na yeye binadamu na ana idara nyingi lakini vile vile shughuli zake hazifanywi katika idara tu moja kwa moja. Waziri shughuli zake zinafanywa mpaka katika maeneo ya kazi. Sasa unapomuuliza swali na swali lile anapouliza mwakilishi inakuwa hakuuliza yeye na ndio maana anasema kwa niaba ya wananchi wangu, ina maana swali lile amelipata aidha katika ziara zake kwenye mikutano ya jimbo au kuna wananchi wamemfuata katika ofisi yake au nyumbani kwake, au wengine wamemfuata Barazani nje kwenye ukuta na kuja kumwambia masuala mbali mbali.

Mhe. Spika, ukiona watu wengi wapo nje katika ukuta wale ndio wanaowapa maswali mengi Waheshimiwa Wajumbe kuja kuuliza humu ndani. Kwa hivyo, wale wasifikiriwe wanakuja kwa nia nyengine. Sasa swali lile Mheshimiwa akishapewa na wananchi wake anatakiwa achukue si chini ya siku 21 amuulize waziri ili na yeye apate ufafanuzi wa kutosha. Lakini Mheshimiwa kasema kwa nini mjumbe yeye aliyeuliza swali hapewi maandishi ya kumwambia kwamba kesho swali lako litaulizwa, au jiandae siku fulani. Sasa hili tunalichukua kwa sababu hili suala letu kama Baraza la Wawakilishi, timu itakaa na tutafanya utaratibu ili waheshimiwa muweze kujua hivyo.

Ni kweli kwa sababu Mhe. mjumbe anapouliza swali akawa hayupo hata yule anayemuulizia swali lile, swali la nyongeza hawezi akalipata vizuri. Kwa

sababu Mheshimiwa anapouliza swali anakuwa ameshalifanyia utafiti na ameshagundua pengine kuna kasoro. Pamoja na kwamba hakuna kasoro lakini alikuwa anataka mambo yenye vizuri zaidi. Sasa kama atauliziwa swali lile na mtu mwengine basi lile la nyongeza linakuwa halina ladha sana kwa sababu yule anaongeza na kwa kubahatisha.

Hata wakati mwengine Mhe. Spika, anawakalisha kitako waheshimiwa pale, anamwambia, hebu hilo swali lako la nyongeza liandikie swali la msingi. Kwa sababu yule aliyeuliza kauliza swali jengine, mwakilishi kwa kuwa lile swali amekuwa na uzoefu nalo na yeye ametaka kuongeza lakini ameongeza sipo. Sasa pale inakuwa lazima arekebishwe awekwe katika utaratibu wa kawaida. Kwa hivyo, hii inaonesha wazi wazi kwamba yule aliyeuliza swali la msingi basi yeye ndiye ataekuwa zaidi swali la nyongeza aliulize na ndio maana Spika anakuwa anampa nafasi ya mwanzo. Kwa hivyo, hili tutaliangalia na tutajitahidi ili wale waheshimiwa kama kesho swali lako litatoka basi leo uweze kupewa barua mapema kwamba hebu kesho jiandae swali lako litatoka.

Mhe. Spika, nikiendelea na ufafanuzi Mhe. Subeit Khamis Faki mwakilishi wa Micheweni jimbo ambalo linapendelewa kwa kila kitu sasa hivi, hata redio kuna Redio Micheweni sasa hivi na kijiji cha millennia. Kwa hivyo, ni jimbo ambalo linapendwa kuliko majimbo yote ya Zanzibar. Yeye vile vile ameuliza maswali yake kwamba Spika anapokuwa katika kiti chake anapoendesha Baraza anakuwa kavaa joho, lakini anaposhuka chini anakuwa si Spika, tena anakuwa Mwenyekiti lakini bado joho analo. Akasema wenzetu kule mimi sijapeleleza sana lakini yeye kasema Bungeni anapokuwa Spika anakuja kwenye kiti chini analivua lile joho.

Lakini hili mimi nafikiri sisi tusiige kila kitu, kwa sababu tukiiga kila kitu mwisho kuna mambo mengine wenzetu wakikosea sasa itakuwa na sisi tunakosea. Sasa Spika anapokuwa juu ya kiti hapa ndio anakuwa na cheo chake cha Spika, anaposhuka chini anakuwa Mwenyekiti na ndio maana hata hili rungu linakuwa limefunikwa.

Vile vile hata sasa hivi tumesharekebisha kanuni hapa, ndio tumo katika marekebisho, tukisharekebisha kanuni Mwenyekiti na yeye anatakiwa avae joho pale. Kwa hivyo, Mwenyekiti akiwa juu ya kiti atakuwa Mwenyekiti, akiwa chini hapa vile vile atakuwa mwenyekiti. kwa hivyo, bado ndio maana nikasema sisi tusiwe na haraka ya kufanya marekebisho katika hili. Kwa sababu Spika ikibidi akavue joho labda tukenda kwenye Baraza letu jipya, lakini sasa hivi itabidi atoke nje kwanza halafu arudi muda unapotea. Lakini bado nafikiri tuendelee na utaratibu wetu Spika, aendelee kuwa na joho lake katika shughuli zake mpaka tunapomaliza.

Lakini vile vile Mhe. Subeit alielezea kwamba katika dua ya kuliombea Baraza tuna dua mbili hapa, lakini yeye akasema kwamba ile *heading* kidogo ifanyiwe marekebisho, kwamba baada ya dua ya kuliombea Baraza na dua ya kuiombea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi iwe dua ya kuiombea Zanzibar tu peke yake.

Mhe. Spika, mimi nafikiri hili wala tusiwe na wasi wasi nalo sana, sijui kuna kitu gani kinachomkwaza yeye hapa, lakini dua zetu naona zinakwenda vizuri. Kwa sababu kuna dua ya kuliombea Baraza na kuna dua ya kuiombea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali ndio inayotuongoza sisi na serikali inapoongoza inakuwa haichagui chama serikali inaongoza watu wote. Kitu kinachoongoza unatakiwa ukiombee dua, kwa sababu unapokiombea dua ndio inapatikana ile neema. Kwa hivyo, serikali ni yetu sote hii na katika serikali hakuna kusema kwamba huyu katibu, mkuregenzi *CHADEMA*, *NCCR* Mageuzi, ya wao kule wala hawajui masuala hayo. Ndio maana hata tunapokwenda katika kamati basi tunapata mashirikiano makubwa sana na huwezi kujua kwamba huyu ana itikadi na huyu ana itikadi gani.

Kutokana na kwamba watendaji wetu ndani ya serikali hawaoneshi utashi wao wa kisiasa na hata sisi tunapokwenda katika kamati tunajitahidi tusioneshe utashi wetu wa kisiasa. Kuna wale wengine watendaji wapya wanauliza hasa, yule aliyeuliza swali lile ina maana yule chama fulani? Tunamwambia ndio, mbona kasema vile. Sasa unamuuliza kwani ulitaka aseme vipi? Nilifikiri atapinga, kwani unafikiri kazi yake kupinga yule, yeye anatengeneza bwana. Kwa hivyo, tunapofanya kazi zetu katika kamati ndio tunaonesha hasa kwamba kule ndio tunafanya kazi hasa ya kusaidia nchi. Watendaji wetu hawaoneshi utashi wa vyama wala sisi hatuoneshi utashi wa vyama.

Isipokuwa hapa katika haya maneno ndio kidogo tunaonesha utashi wa vyama lakini tunapokuja katika kazi zenyewe ule utashi wa vyama unaondoka na huu ndio umahiri wa Baraza letu la Wawakilishi. Tofauti unavyoliona juu lakini ukija ndani mambo kidogo yako tofauti. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nadhani hili Mhe. Subeit lisimtilie hofu naona mpaka sasa hivi hizi dua zetu zinakwenda vizuri. Na tunashukuru mafanikio yote tunayoyapata ndio hizi dua ambazo kila siku asubuhi tunakuwa tunaziomba.

Mimi kuna siku moja Mhe. Spika, kuna shekhe fulani niliwahi kumuuliza swali. Kwa sababu katika baadhi ya misikiti yetu kuna wengine wanamtaja kiongozi wa nchi na wengine huwa hawamtaji. Sasa kuna mmoja nilimuuliza kwa nini nyinyi mnataja kiongozi wa nchi lakini kuna misikiti mingine hawataji kiongozi wa nchi. Unajua ni uelewa, kwa sababu elimu inatakiwa wewe usiilete na utashi wako, elimu inatakiwa uwe na upeo mkubwa. Kwa mfano, mnaweza kuja kumpata kiongozi jahili, sasa kiongozi yule kama

hamumuombei dua yule ule ujahili utazidi, lakini kama mtakuwa mnamuombea dua kama kiongozi jahili.

Unajuwa Mwenyezi Mungu dua yoyote anaipokea, sasa ile dua ina mambo mawili, kwamba anaipokea na kama anaifanyia kazi pale pale au anaiweka, unaweza ukamuombea dua mtu leo lakini lile ulilomuombea akaja akalipata mwaka ujao. Sasa dua yoyote inapokelewa, tunatakiwa kitu usichokipenda basi ndio ukiombee dua, kwa sababu kila ukikiombea dua kitabalika baadae utakuja kukipenda. Kwa hivyo, hii ilikuwa ni hikma na ilmu niliipata na ndio maana ukaambiwa kwamba adui mpende, adui ukimpenda utakuwa unapunguza idadi ya maadui.

Mhe. Spika, unajua kuombea dua kitu sio ukiombee kile unachokipenda tu, hata usichokipenda unatakiwa ukiombee dua vile vile. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hapa nilikua natoa ufafanuzi na ilmu kidogo niliyoipata na mimi nikaona ile ile ilmu ndogo niliyoipata na mimi niwapatie wenzangu.

Mhe. Mohammed Ali Salim wao mambo kama hayo ndio wanayoyajua, ndio watoa fiqhi na mambo kama hayo. Kwa hivyo, hili nilitaka nilitolee ufafanuzi wa hilo kwamba tusiwe na wasi wasi nalo katika utaratibu wa dua zetu na mambo mengine.

Lakini vile vile Mhe. Mohammed Ali Mula kuna mheshimiwa mmoja kambatiza jina anamwita *Mr. Correction*. Mhe. Mula unapozungumza basi ujitahidi sana japo koma atakuja kukwambia pale uliposema koma huku-*pause*, ulikuwa unaendelea tu. Sasa lakini hii inaonesha ni namna gani anavyokuwa makini katika kufuatilia shughuli zetu.

Kwa hivyo, ame-*quote* kifungu cha 114(4) anasema kwamba, pale neno majibu iwe mujibu. Nafikiri hili tutajaribu kuangalia, hata katika marekebisho kuna mambo mengi kwenye *typing error* yalijitokeza, lakini hapa inakuja katika ufasaha wa lugha. Kwa hivyo, hili tunalichukua.

Kuna suala jengine pia alisema kwamba kuna marekebisho ya neno itawasilisha katika kifungu cha 117(3). Alisema itawasilisha iwe itawakilishwa. Kwa hivyo, na hili kama tulivyosema humu tuna wataalamu wengi, tuna wasamiati wa Kiswahili, tuna watu wa Fiqhi humu, tuna watu wa dua. Siku moja kuna mheshimiwa mmoja alipinduka hapa akapigiwa dua hapo hapo aliinuka, kwa hivyo Baraza hili limejitosheleza kwa wataalamu wa aina zote. Kwa hivyo, hili Mhe. Mula tumelichukua na tutaliangalia katika marekebisho yetu haya kasoro kama hizi zisijitokeze. Hili moja sitaki nilirejee kwa sababu Mheshimiwa aliyetoa hoja alijaribu kulitolea ufafanuzi sitaki tulirejee tena.

Vile vile Mhe. Hamad Masoud yeye aliomba nyongeza katika kanuni yetu ambayo hajaiona. Anasema mara nyingi mawaziri anapoona ngoma nzito anasema nitakujibu kwa maandishi. Sasa kwa kuwa hakuna utaratibu wa kanuni waziri inayombana kwamba ndani ya siku fulani yale maandishi ameshayatoa basi wakati mwengine waziri yule huona ndio imetoka, kama alivyosema. Kwa sababu Mheshimiwa akishauliza swali akishajibiwa hata kama umemjibu sivyo tena kabakia kutoa macho tu hana la kufanya. Lakini sasa kama kanuni itambana basi lile swali alilouliza kama hakulipata jawabu yake, na kwa sababu wakati mwengine waziri hasa suala ambalo linahitaji takwimu anatakiwa lazima alilete kwa ufasaha kabisa.

Mhe. Spika, pengine yule anayeuliza yeye ameshafanya *research* na ana takwimu sahihi, sasa unapomletea majibu ambayo hayana takwimu nzuri pale pale anaweza akakupiga buti akasema kwamba unalipotosha Baraza na itabidi kanuni uchukue mkono wake. Sasa ndio maana waziri wakati mwengine anapoona hii ngoma nzito anasema nitajibu kwa maandishi.

Mimi nakubaliana na hii hoja kwamba ndani ya kanuni yetu tuweke sasa muda wa kujibu kwa maandishi. Kwa sababu inawezekana waziri kaulizwa swali leo kesho sisi tunategemea kuahirisha Baraza, sasa mfano waziri akipewa siku mbili au tatu kikao kitakuwa kishaahirishwa. Mimi nadhani kama limeulizwa swali leo basi waziri apewe uhuru kama anaweza kutoa ndani ya siku ile ile au ya pili yake, lakini kuwe na kikomo isizidi kupitisha katika kikao kitakachofuata. Kwa mfano hakuweza kujibu leo na kesho pengine wiki nzima kama anahitaji kwenda kufanya utafiti zaidi huko chini. Kwa sababu kuna mambo mengine ni mambo ya wananchi kama mimi na Mhe. Omar Ali Jadi siku zote tunasokotana, shilingi 12 milioni zimejengewa mabanda ya kuku, namwambia aa nimekwenda yamejengwa.

Sasa kuna mambo inabidi ukishaulizwa unasema hebu ngoja niende inabidi uangalie. Sasa kwa kusema nitakujibu leo unapiga simu pengine na wewe waziri unapotoshwa unakuja kusokotana na mwakilishi kwa mambo ambayo hayana msingi. Kwa sababu msokotane kwa mambo ya msingi, lakini kwa mambo yasiomsingi inatakiwa waheshimiwa wawe wanaridhika. Sasa mimi nadhani katika marekebisho ambayo tutayafanya sote tuje tukubaliane kwa pamoja waziri na yeye apewe uhuru, kama anaweza kutoa jawabu ile ndani ya kikao kile lakini kisizidi kikao kinachokuja. Kwa hivyo, kabla ya kikao kinachokuja lile jawabu awe ameshalitoa.

Swali anapouliza mwakilishi lile linakuwa sio lake yeye, ile jawabu inatakiwa na wengine pia waweze kuipata. Kwa hivyo, utaratibu katibu atakuwa yeye anasambaza jawabu kwa swali alilouliza Mhe. Kwa hivyo, Mhe. Hamad

nyongeza hii mimi nakiri tunaikubali na kwa sababu itatusaidia katika kutuweka makini na sisi katika kusimamia majukumu yetu.

Mhe. Spika, kuna masuala mengine sitaki niyarejee rejee kwa sababu nimeshayatolea ufafanuzi na kwa sababu muda unakimbia kuna wengine walijaribu kuniuliza maswali kwa maandishi, lakini nadhani haya yote ambayo yaliulizwa kwa maandishi ingawa waheshimiwa wengine hawakuandika majina yao, lakini nadhani nilipokuwa nikijibu nimejaribu kujitahidi kuyaoanisha kwa pamoja.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Tunakwendaje? Kuna mengine yamerekebishwa ndani ya marekebisho na kuna mengine yamebakia kama yalivyobaki. Huu si mswada, sasa tukihisi kwamba ni vyema tukenda kifungu kwa kifungu tunaweza tukaita hata Kamati ya Baraza Zima ili tuhakikishe kifungu baada ya kifungu tunakubaliana. Na kama tunaridhika moja kwa moja na haya yaliyokwishatolewa basi tutamaliza moja kwa moja.

Lakini hoja imetolewa niwahoji waheshimiwa wajumbe wale wanaokubaliana na rasimu hii pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono.Wanaokataa, waliokubali wameshinda. Inaonekana mambo yamemalizika moja kwa moja, niwashukuru basi waheshimiwa wajumbe na sasa tunaendelea.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe nimepokea maombi kuhusu shughuli inayoendelea hapa hoja za wajumbe, ambapo tunamtarajia Mhe. mjumbe za Baraza hili kutoka Jimbo la Mkanyageni awasilishe hoja binafsi. Hili suala ni kubwa na muhimu sana, ombi nililopokea ni kwamba tupate nafasi ya kulizingatia.

Mhe. Subeit Khamis Faki alikuwa anasema hapa tulikuwa tuna utaratibu wa kukaa kama njama wakati mwengine. Kwa uzito wa suala hili upande wa kulia yangu waliniomba wapate nafasi kuliangalia suala hili na nikasema kwa kuwa jambo limeingia katika *order paper* hii nitaweza kuliamua kwamba tufanyeje, isipokuwa tuliamue ndani ya ukumbi huu. Lakini ni kwamba tupate muda ili suala hili liweze kuwasilishwa jioni. Kuwasilishwa litawasilishwa kwa sababu limeingia katika *order paper,* kulikuwa na maombi labda iwe kesho nikasema

sasa kama *order paper* imeshaonesha kwamba leo basi tulimalizeni leo. Lakini tuone hili suala la kama tulisikilize jioni au laa. Sasa kazi hii nisiifanye mimi wale walioniletea maombi mmoja aseme ili tuone kama tulifanye jioni au sasa hivi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kutoa hoja kwamba hoja hii ya Mhe. Haji Faki Shaali vizuri tukapata muda mzuri wakati wa jioni ili tupate wasaa mkubwa zaidi. Kwa sababu hoja kama hii haitakiwi kuwa inatolewa halafu baadae tunaahirisha Baraza, hata ile ladha inapungua kidogo. Lakini kama nilivyosema kuwa kuna baadhi ya mambo ni mambo ya kikatiba lakini vile vile kunahitajika takwimu sahihi.

Vile vile hoja hii inatakiwa mazingatio makubwa tusije tukafanya kazi ambayo pia itakuwa sio yetu. Kwa hivyo, kwa maoni hayo naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu uliahirishe hadi saa 11:00 jioni.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mimi Mhe. Spika, naomba muongozo wa kiti chako. Mjumbe anapoleta hoja hii kanuni inaagiza hatua zipi zifanyike mpaka kuwasilishwa kwake hata leo ikabidi tuambiwe iahirishwe. Naomba muongozi wa kiti chako tu.

Mhe. Spika: Kanuni inahitaji kwamba suala kama hili baada ya hoja kutolewa kwa maana ya mtoa hoja kuwasilisha hoja yake, basi ipigwe kura juu ya lile ombi ambalo limo. Ombi ni kwamba kamati teule iundwe ndio ombi liliomo ndani ya maelezo ya hoja hii. Kamati teule iundwe kwa madhumuni ya kuchunguza mambo ambayo Mhe. Mjumbe uliyataja na yamo katika maelezo ya hoja hii. Sasa suala la ombi ambalo hasa nimelipata kwamba suala hili ni kubwa sana, ni zito na ni muhimu.

Mimi nalikubali kwamba ni kubwa na ni muhimu. Sasa kupata upande mmoja ukatoa maelezo kwa maelezo kama yaliyomo ndani ya hoja hii halafu ikapigwa kura kidogo panakuwa na tatizo. Walichoniomba upande wa kulia yangu ni kwamba wapate muda ili hili jambo waliangalie. Kuwasilishwa itawasilishwa bila ya wasi wasi, hatua zake zitafuatwa kama zilivyo kwa kadiri tutakavyoona inafaa, lakini hoja ilikuwa ni kwamba wapate muda na wao waliangalie. Labda nieleze ile hali halisi iliyotokea. Kabala ya utaratibu, Spika anaposimama mwachieni aseme.

Kilichotokea ni kwamba Kamati ya wawakilishi wa chama kinachotawala ilitaka iangalie hili suala. Kwa bahati jana mimi nilikuwa sipo tulipata msiba na wenzangu wakawa wameendelea na kazi ikafanyika kazi . Niliporudi nilipita hapa ili kusikiliza kama kamati imekaa au laa, nikaambiwa shughuli

zimekwisha. Katibu akanipigia simu jioni ili kujua je, shughuli hii inaingia katika *order paper* au laa? Nikamwambia iweke ndani ya *order paper* ili shughuli hii ifanyike kesho kwa maana ya leo.

Asubuhi mapema kumbe ile Kamati ya Wawakilishi haikufanyika ndio nikapata hilo ombi kwamba tupate muda kipindi hiki baada ya kumaliza shughuli hizi wakae ili hatimaye hoja hii iwasilishwe jioni. Nikasema kwa kuwa tayari jambo hili liko ndani ya *order paper* na lishughulikiwe kwa mtiririko kama ulivyo ndani ya *order paper,* basi wacha tuliamue ndani ya Baraza. Je, jambo hili linaweza kufanyika sasa hivi au hoja itatolewa kuahirisha hadi jioni ili suala hili liwasilishwe? Hicho ndicho ambacho nimekisema na nadhani sijui kama alisema kwamba natoa hoja!

Sasa hapa ilikuwa tuiamue hii hoja aliyoombwa kwa maelezo hayo aliyotoa kuwa suala hili liahirishwe mpaka jioni ili Kamati ya Wawakilishi wa CCM kama ile aliyozungumza Mhe. Subeit kuwa tunakaa ndani ya kamati huku wanakaa na huku wanakaa. Kwa madhumuni ya kwamba suala hili maelezo ya humu yamo siyasomi Mheshimiwa utapowasilisha utayasoma, lakini je, itoshe baada ya hapo kwamba tupige kura au laa? Sasa wenzangu wa upande wa mkono wa kulia kwa maana wawakilishi wa CCM wameniomba upatikane muda huo nikasema basi tutaamua ndani ya Baraza suala hilo la kwamba ama tulifanye sasa hivi au tuliamue hapo jioni. Ndio Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi akatoa hoja hiyo, itakuwa ni hoja juu ya hoja lakini ni kuhusu mtiririko, iwe sasa hivi au jioni.

Sasa mimi ningeomba tulizingatie suala hili kwa sababu ni suala ambalo ni kwa faida ya nchi hii, ni kwa madhumuni ya nchi hii, si suala la Mhe. Haji Faki Shaali ambaye ameomba kutoa hoja hii kuwa ni lake binafsi hapana, hili ni suala la nchi. Kupata nafasi tukawa na mazingatio na hatimaye tukaamua ipasavyo, vilivyo, vizuri, nadhani ni jambo la maana. Lakini nyinyi ndio mtaosema kwamba iwe hivyo au laa. Sasa nitapokaa kitako nitawauliza kama hoja ile inakubaliwa au haikubaliwi kwa ajili ya suala hili kuitishwa jioni, lakini kuitishwa litakuwepo kama linavyoonekana katika *order paper* hii.

Wajumbe niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Kwa hivyo, bado marekebisho ya kanuni hayajafanyika. Sisitishi moja kwa moja mpaka Baraza lijalo ndio nitafanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza lako tukufu hadi saa 11:00 jioni. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni tena kwa mashirikiano na sasa naahirisha kikao hiki mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA WAJUMBE

Hoja ya kuliomba Baraza kuunda Kamati Teule ya Baraza kwa Mujibu wa Kanuni ya 115, Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2007

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa jioni hii kunipa fursa hii adhimu. Pia sina budi kuwashukuru wenzetu wa Chama Tawala kwa kutuomba upande wetu kwamba tuwape fursa kwenda kubadilishana mawazo kuhusu suala hili kama wewe mwenyewe ulivyosema kubwa.

Mhe. Spika, ni imani yangu kama ulivyotangulia kusema wakati wa asubuhi kwamba suala hili ni letu, si langu, kwa maana hiyo litahitaji mazingatio kama ulivyosema wewe asubuhi, kwa kuangalia maslahi ya nchi na sio maslahi ya mtu.

Mhe. Spika, sasa nakuja katika maelezo ya hoja yenyewe. Mhe. Spika, wajibu wa Serikali pamoja na vyombo vyake ni kufuata misingi ya uhuru, haki na amani kama Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (Toleo la 2003) inavyoeleza katika kifungu cha 8.

Mhe. Spika, katika kuyatekeleza haya Katiba imeweka bayana katika kifungu cha 12 (1) juu ya usawa mbele ya sheria na katika kifungu cha 12 (4) ikaweka katazo la kubaguliwa mtu na yeyote anayefanya kazi chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi ya ofisi yoyote ya serikali au uongozi mwengine wa chama chochote na vyombo vyake.

Mhe. Spika, haki za lazima na uhuru wa mtu binafsi zisiposimamiwa ipasavyo, kinachofuatia ni vurugu na wananchi kupoteza imani na serikali yao. Baraza la Wawakilishi likiwa ndio msimamizi wa shughuli za umma kama inavyoeleza kifungu cha 5A (2) (Katiba ya Zanzibar ya 1984) lina wajibu wa kudhibiti mwelekeo wowote mchafu ambao unaweza kuleta maafa katika nchi.

HOJA YENYEWE:

BASI KWA KUWA Katiba ya Zanzibar ya 1984 (toleo la 2003) inakataza ubaguzi wa aina yoyote kama ukabila, jinsia, pahala mtu anapotokea, mwelekeo wa kisiasa, rangi au dini,

NA KWA KUWA kumejitokeza malalamiko mengi ya wananchi Unguja na Pemba ya kubaguliwa na kunyimwa vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi kinyume na Sheria Nam. 7 ya 2005,

NA KWA KUWA walalamikaji wanadai kwamba sifa za kupewa vitambulisho wanazo,

NA KWA KUWA chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Nam. 7 ya 2005 vitambulisho hivyo vina ulazima katika kupata huduma mbali mbali za kijamii na vitatumika pia katika uchaguzi,

NA KWA KUWA chini ya kifungu cha 14 (1) cha Sheria Nam. 7 ya 2005 ni kosa la jinai kutokuwa na kitambulisho kwa mwenye sifa ya kuwa nacho,

NA KWA KUWA, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amekwishatoa wito wananchi wote wenye sifa wapewe,

NA KWA KUWA suala la kuwanyima wananchi wengi vitambulisho hivi limekwishaleta matatizo ya kisiasa katika nchi yetu,

HIVYO BASI ili kuirejesha nchi katika hali ya utulivu na amani na kujenga udugu wa dhati kwa wananchi wetu mimi HAJI FAKI SHAALI naomba kutoa hoja binafsi ya kulitaka Baraza hili tukufu chini ya kifungu cha 115 (1) cha Kanuni za Baraza liunde Kamati teule kwa ajili ya:

(a) Kuchunguza malalamiko ya wananchi kunyimwa vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi *ilhali* sifa za kupewa wanazo.
(b) Kuchunguza tuhuma kwamba kuna watu wasio na sifa ya kupewa vitambulisho hivyo lakini wanapewa.
(c) Kuchunguza na kupendekeza mambo mengine ambayo yatakuwa na manufaa kwa Baraza letu na nchi kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha na naomba Baraza lako tukufu likubali hoja na kuchukua hatua muafaka. Nashukuru sana ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Mjumbe amewasilisha hoja yake kwa kutumia kifungu cha 115 cha kanuni. Na kwa kuwa kifungu hiki kinataka kwamba Kamati Teule inayoundwa hapo au hoja hiyo isipate nafasi ya kujadiliwa.

Lakini Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu kwa kuwa hoja hii ni muhimu kwa maslahi ya taifa, na kwa kuwa ni hoja ambayo imewagusa wananchi. Naomba Baraza lako likubali kutenga kanuni kando kufuatia kifungu cha 150 ili hoja hii Waheshimiwa Wajumbe wapate kuijadili. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kumekuwa na hoja hizo mbili, hoja moja ya Mhe. Haji Faki Shaali na hoja ya pili ambayo hoja hii chini ya kifungu hiki kama alivyoeleza Mhe. Salmin Awadh Salmin ni kwamba hoja kama hii chini ya kifungu hicho 115 haitaki kujadiliwa.

Sasa anachosema Mhe. Salmin Awadh Salmin ni kwamba kwa uzito na umuhimu wa jambo hili basi tutenge kanuni kando, hii kanuni inayosema kwamba isijadiliwe tuitenge kando na badala yake yeye anasema kwamba hoja hii tupate mjadala kidogo kabla ya kufikia maamuzi ya hoja hii.

Sasa hoja juu ya hoja. Maana yake hapa hoja ya Mhe. Salmin Awadh Salmin inatuzuia tusimalize shughuli hii kwa sababu ni *process* ile mpaka tuamue hoja yake ili tufikie pahala tuseme sasa kama tujadili au tusijadili kwa kutenga kanuni kando. Hicho ndio anachokizungumza kwamba tupate nafasi ya kujadili badala ya kuamua baada ya maelezo haya ya hoja aliyoyatoa Mhe. Haji Faki Shaali katika hoja yake aliyowasilisha punde, ndio maana yake. Kwa sababu ni *process* itabidi tuamue hili halafu twende kwenye hoja inayohusika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, mimi sipingani na Mhe. Salmin Awadh Salmin lakini nataka mwongozo wa kiti chako utusaidie sisi wenzako.

Unapotenga kando kanuni kuna hoja ndogo 52 (1) nadhani labda niisome, au bora mtiririko mzuri niisome ile ya mwanzo.

> "Kwa idhini ya Baraza yoyote kati ya kanuni hizi yaweza kutengwa kando kwa madhumuni makhsusi baada ya mjumbe yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo". Ndio kama alivyofanya Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Spika, pili inasema "Hoja inayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii haitotolewa taarifa na itaamuliwa bila ya mabadiliko wala mjadala wowote".

Nadhani ndio sasa hivi hapa labda tulipo kwamba itaamuliwa bila ya mjadala wowote.

Mhe. Spika, tatu inasema "Maelezo ya hoja yoyote ya kutaka kutenga kando kanuni yoyote yatakuwa ni pamoja na maelezo kuhusu madhumuni ya kutaka kanuni itengwe kando".

Sasa nadhani hapa mimi kidogo panaanza kunitatiza yale madhumuni ya kutaka kutengwa kando kanuni hapo kidogo sijaelewa.

Mhe. Spika, nne "Kanuni yoyote inayotengwa kando itatengwa kando kwa madhumuni yaliyokusudiwa tu kwa kutengwa kando huko na sio kwa madhumuni mengine yoyote".

Mhe. Spika, nadhani tusaidie hapo.

Mhe. Spika: Labda nirudie alichokisema Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba hoja hii chini ya kifungu hiki hii hoja ambayo iko mbele yetu hivi sasa ni hoja ambayo haihitaji kujadiliwa. Baada ya hivi ulivyokwisha iwasilisha basi niwaulize Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali hoja wanyanyue mikono, wanaokataa hoja, waliokubali au waliokataa wameshinda. Hoja gani hiyo, ya kuunda Kamati Teule kwa sababu ndicho kinachohitajika hapa.

Sasa anachosema Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba kwa uzito na umuhimu wa jambo hili ingefaa basi tujadili, lakini tukijadili maana yake sasa hii kanuni inayotutaka tusijadili tuitenge.

Kwa hiyo, yeye kwa kutumia kifungu kile cha 150 ndio anasema mimi naomba nitoe hoja kwamba tuitenge kanuni kando hii ya 115 inayotaka hoja hii isijadiliwe na badala yake tuijadili halafu twende kwenye maamuzi. Hii ndio ile iliyokuwa haitaki kutolewa taarifa, taarifa yake ndio ile aliyoisema tu hapa.

Maana hii ya kwako ilikuwa inahitaji taarifa, taarifa ulileta mapema imetimia siku mbili na sikuileta mapema kutaka iive kwa zile siku mbili kama taratibu zilivyo.

Sasa kwa mujibu wa tarehe uliyoileta mpaka hii leo, leo imeingia nadhani siku ya tatu au ya nne. Kwa hiyo, imeiva kikamilifu kwa sababu zile siku zinazohitajika kwa mujibu wa kanuni zipo zimetimia na taarifa kama ulivyoleta ipo imetimia.

Sasa anachokisema kwamba tusiende hivi hivi kimya kimya kwamba maelezo haya kwa uzito wa hili jambo lenyewe hapana tujadili kidogo na baadae uje ufanye majumuisho kama kawaida, halafu useme kwamba sasa naomba kutoa hoja baada ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe huku na huku.
Maana tukishaamua kwamba ijadiliwe sio kwamba watajadili huku tu hapana, huku watajadili na huku kama kuna wajumbe nao pia watajadili, ndivyo ilivyo hivyo.

Sasa madhumuni makhsusi ni kwamba suala hili ni zito, kwa hiyo kanuni hii ya kutaka isijadiliwe tuitenge kidogo ili twende kwenye mjadala ili ieleweke tunachohitaji ni nini na kwa sababu zipi. Tumo katika semina ndogo ya kuelimishana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa mujibu wa mtoa hoja kilichohitajika ni kutafutwa ukweli. Kwa hivyo, haupatikani humu kwa mjadala, utapatikana kwa hiyo kamati huenda ikapewa huo ukweli.

Kwa sababu kinachohitajika ni kuonekana kwamba wapo ambao wamepewa vitambulisho na wapo wengi ambao hawajapewa vitambulisho na wanastahiki. Sasa kama hiyo kamati haijafanya kazi tutajadili nini?

Mhe. Spika: Maelezo haya tuliyoambizana ndio hayo ya kujadili ili kufikia kwamba kweli kufuatana na maelezo yaliyotoka hapa zaidi ya haya? Maana haya ni ya Mhe. Mjumbe mmoja huyu hapa Mhe. Haji Faki Shaali, haya ni maelezo yake binafsi. Sasa wajumbe wanasema hapana tueleweshane kwa kujadiliana ili tufikie maamuzi ya kusema kwamba sawa Kamati Teule iundwe au la.

Taratibu zinakuja vile vile kama zinavyokuja hoja nyengine kwamba baada ya mjadala huo ambao nafikiri hautakuwa mrefu, halafu utafanya majumuisho mtoa hoja kujibu kwa mujibu wa vile unavyoiona kwa mtazamo wa hoja yako. Baadae utamalizia kama wanavyofanya benchi ya mawaziri hapa, utasema baada ya hayo sasa naomba kutoa hoja. Maana yake unaendelea kusisitiza hoja yako hii sasa hapo kwa sababu kila mmoja ameshapata mwelekeo kutokana na

maelezo ya huku na huku, tutaamua wanaokubali hoja wanyanyue mikono, wanaokataa.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nadhani asubuhi mimi na wenzangu tulifikiria kwamba pale mlipotuomba muda labda mnakwenda kujipanga na nilijua umuhimu wa kukutana Kamati ya Chama mimi naufahamu. Mimi ni Mnadhimu ndio wenzangu wakanambia uwe Mnadhimu.

Ninafahamu umuhimu wa suala hili, Mheshimiwa wewe kama Spika, kulipeleka kwa chama chako. Hilo haliwezekani wewe hoja ukakurupuka tu kuja hapa. Mimi nilikubali kwa sababu hata kama mimi ningekuwa ni Spika lakini si imetokea kwenye chama.

Lakini Mhe. Spika, mimi nilileta hoja hii sikubaliani hata kidogo na wazo la kutengwa kando kanuni kwa sababu mjadala wetu utaathiri kazi ambayo tutataka kwenda kuifanya. Kwa kuzingatia hilo naondoa hoja yangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imeondolewa.

UTARATIBU

Mhe. Haji Omar Kheri: Mhe. Spika, mtoa hoja ameamua kuondoa hoja mwenyewe. Kanuni hizi ndio maana zina vifungu 155 na leo tumepitisha marekebisho ya kanuni kwa madhumuni ya kufanya utendaji wa kazi zetu uwe bora zaidi. Huwezi ukang'ang'ania kifungu kimoja cha kanuni ukataka kifungu kingine kilichopo katika kanuni hizi kisitumike.

Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe alieleza shutuma dhidi ya serikali iliyopo madarakani. Haiwezekani tuje hapa tumsikilize atoe hoja, halafu tunyanyue mkono, *definitely* tungeweza kushinda CCM. Lakini lazima tulitakiwa tutoe ufafanuzi juu ya yale ambayo aliyasema.

Sasa kwa misingi hiyo, ni kwamba ameondosha hoja pengine baada ya kuona kwamba hoja yake itapata majibu kabla ya hilo ombi la kuunda Kamati Teule halijakubaliwa.

Mhe. Spika: Tunatafuta nini na hoja haipo. Shughuli za mkutano huu zimekwisha. Kama ingekuwa Mhe. Waziri Kiongozi ulimwambia mapema kama shughuli zinamalizika leo ningemwita aka-*wind up,* lakini tulipanga kesho kwamba tumalize shughuli hii na hiyo kesho tena tuliweka kwamba labda inawezekana ikawa jioni hatujajua shughuli hii itatufikisha wapi. Sasa Katibu wangu ananambia taarifa shughuli za leo zimekwisha, kwa hiyo baada

ya hoja hii kuondoka shughuli za leo zimekwisha. Sasa tunasema tunatafuta nini tena. *(Kicheko)*

Kwa hiyo niweke usawa? Kuna taarifa gani?

UTARATIBU

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kututendea haki kwa sababu ilikuwa Mhe. Mjumbe aliyekaa kitako asiseme kitu itolewe hoja tumalize kwa sababu shughuli za leo zimemalizika. Lakini kwa sababu alipata fursa na sisi tulitaka kusisitiza kwamba kwa mjadala wa hoja ambayo ilitolewa hapa ungelifanya kama mfano wa Mahakamani kuwa ushahidi tayari umeshatoka kwa hiyo unakuwa umeua kesi. Ndio sababu inayotufanya sisi tukatae na tusione uzito wa suala la kujadiliwa hoja hii hapa. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kuweka sawa hiyo na kuweka msimamo wetu kwamba hoja ingejadiliwa hapa ingelikuwa tunaua ushahidi.

Mhe. Spika: Nashukuru taarifa ya Katibu wangu hapa anasema shughuli zimekwisha. Nawashukuruni Waheshimiwa Wajumbe wote mliopata nafasi.

KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pamoja na kwamba nilisoma marekebisho ya kanuni kwamba tutakuja kukupa uhuru uweze kuahirisha Baraza bila ya kutuhoji. Lakini kwa kuwa kanuni ile tutakuja kuitumia katika kipindi kinachofuata, naomba sasa uliahirishe Baraza lako tukufu mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 30 Oktoba, 2009 saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nilifikiri ule utani wa kwamba tuendelee na kazi wakati hazipo ungekuja leo.

Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano katika shughuli zetu za kuendesha mkutano huu. Nilitafuta taarifa kwa Mhe. Waziri Kiongozi akanambia kwamba yeye yuko tayari kuweza kufunga mkutano huu kesho asubuhi. Kwa maana hiyo, kwa kuwa hatuna maswali hiyo asubuhi, kama alivyosema waziri pale shughuli zetu ziende mpaka kesho asubuhi kwa sababu Waziri Kiongozi yuko tayari kuweza kutoa hoja ya kuahirisha mkutano huu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 11:23 jioni Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 30/10/2009)